## MWANAFUNZI adaiwa kumuua mwalimu kwa kisu

UKURASA 2



## RIPOTI MAALUM
Matumizi gesi yalivyookoa mamilioni shuleni

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581379

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


UKURASA WA 3

### RAIS ARIDHIA HEKTA 18,000 KUTOLEWA KWA WANANCHI


RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia kumegwa eneo la Ranchi ya Kagoma iliyoko katika wilaya za Muleba na Karagwe mkoani Kagera lenye ukubwa wa hekta 18,031 kwenda kwa...



UKURASA WA 3

### TAHADHARI ULAJI NYAMA, UNYWAJI MAZIWA MABICHI

UNYWAJI wa maziwa yasiyochemshwa na ulaji wa nyama zinazotokana na ndege ambavyo havijaivishwa vizuri, vimeelezwa kuwa ni hatari kwa afya ya binadamu na walaji wanaweza kuambikizwa maradhi...



UKURASA WA 5


### MIPANGO YAWEKWA KUIMARISHA USAFIRI TANZANIA, DRC

Waziri wa Fedha. Dk. Mwigulu Nchemba, amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)...



# Malumbano ya Bandari yamchefua Askofu

UKURASA 2



Askofu Peter Konki

## Mkutano wa wakuu AU neema tele kwa Tanzania

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akimsikiliza Muuguzi wa Kituo cha Afya Lilambo, Manispaa ya Songea, Ruvuma, Lightness Masasa (kulia), akielezea huduma zinazotolewa wakati wa kumpokea mgonjwa anayefika kituoni hapo, baada ya kuzindua kituo hicho jana. **PICHA: OMR**

## Mganga mbaroni madai ya wizi wa dawa na vifaa tiba

UKURASA 2

MICHEZO YANGA NJOONI 'TUINJOI' UK. 24 KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na waumini wa dini ya Kiislam, baada ya kumalizika kwa Ibada ya Sala ya Ijumaa katika Masjid Imam Abu Ubaida Muslim Bin Abii Kareema Al Tamimi Fuoni, wilayani Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Malumbano bandari yamchefua Askofu

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, amewashukia watu wanaotumia matusi kutetea uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kuacha tabia hiyo mara moja.

Badala yake ameishauri serikali iwakutanishe wadau mbalimbali ili kutafuta mwafaka wa jambo hilo kwa maslahi ya taifa kuliko kuendeleza ubabe wa maneno ambao unamuumiza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Askofu Konki alitoa ombi hilo kwa serikali jana wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya sakata la uendashaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema watu wanaoendelea kuzungumzia sakata la bandari wanamchosha Rais na kumfanya awaze suala hilo tu.

Ili kumaliza malumbano ya jambo hilo, alishauri pande zote mbili wangekutanishwa na kukaa meza moja kujadiliana kwa kuongozwa na wanasheria na wataalamu wa bandari watatoka na majibu sahihi ya kulisaidia taifa.

"Sioni mtu anayemsaidia Rais, iwe Chama Cha Mapinduzi (CCM) uwe upinzani Zaidi ya kuvutana tu. Pia hakuna elimu inayotolewa kwa matusi maana huwezi kumtukana mtu ukasema umempa elimu," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema kelele zinazopigwa na wanasiasa na watu wengine maarufu zinawadhalilisha Watanzania wote.

Konki alisema iwapo serikali itakubali kuyakutanisha meza moja makundi yanayopiga kelele yakajadili suala hili na kupata mwafaka, wao wataamua wakiona mkataba uendelee jinsi ulivyo au uvunjwe ili kusaidia kuliunganisha taifa badala ya kulibomoa kwa kelele.

Alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia kwa kimya na kuacha kujibizana juu ya jambo hili na kwamba hiyo ndiyo busara ya kuwa kiongozi kwa kuwa maana asingeweza kumjibu kila mtu hadharani.

Pia alisema kama Rais alikosea kwenye uwekezaji huo ni binadamu, hivyo anatakiwa kukosolewa na kushauriwa kwa busara badala ya kelele zinazoendelea.

# Mwanafunzi adaiwa kumuua mwalimu kwa kutumia kisu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Qiblaten, iliyoko Kawe, Kinondoni, kwa tuhuma za kumuua mwalimu wake.

Inadaiwa kwamba mwalimu huyo alikuwa akiwahimiza wanafunzi alfajiri kuhudhuria ibada ndipo mwanafunzi huyo akafanya kitendo hicho.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana na kumtaja mwalimu huyo ni Hassan Mohamed (21). Mwalimu huyo alikuwa msimamizi wa wanafunzi kwa upande wa wanaume shuleni hapo.

Alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kumshambulia mwalimu wake kwa kisu shingoni ambaye baadaye alipoteza maisha. "Mtuhumiwa huyu alitekeleza mauaji hayo Julai 20, mwaka huu, saa 11:30 alfajiri baada ya kumshambulia mwalimu aliyekuwa akiwahimiza wanafunzi wakati huo kuhudhuria ibada ya alfajiri," alisema.

Alisema mwalimu huyo alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala na mwili wake umehifadhiwa hospitalini hapo.

Kamanda Muliro alisema mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# Mganga mbaroni madai wizi wa dawa, vifaa tiba

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

MGANGA Mfawidhi wa Zahanati ya Ipoloto, Mbozi mkoani Songwe, Lyoba Nyamosi (34), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuiba dawa za binadamu na vifaa tiba katika zahanati hiyo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Rashid Ngonyani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mtumishi huyo alikamatwa Julai 19, mwaka huu, kwa ushirikiano kati ya jeshi hilo na wananchi.

Alisema mtumishi huyo alikamatwa baada ya kushtukiwa na wananchi akiwa na wenzake wawili ambao walitoroka wakiwa na bodaboda mbili. Alisema baada ya kupekuliwa alikutwa akiwa ameficha dawa hizo kwenye mifuko ili zisionekane kirahisi.

"Julai 19, 2023 majira ya saa 7:00 usiku mtuhumiwa alifika katika zahanati hiyo akiwa na gari dogo kwa nia ya kuiba dawa na vifaa tiba.

Kabla ya kubeba, wananchi walimzingira na kufanikiwa kutoroka na gari," alisema Kamanda Ngonyani.

Aliongeza kuwa baada mtuhumiwa kushindwa kutekeleza mpango wake, alirudi kwa mara ya pili siku hiyo ya tukio majira ya saa 10:00 alfajiri akiwa na wenzake wawili kwenye bodaboda mbili.

"Kama haikutosha, majira ya saa 10:00 alfajiri, mtuhumiwa alirudi tena kwenye zahanati hiyo akiwa na bodaboda mbili. Kwa kuwa wananchi tayari waliweka mtego walifanikiwa kuwaweka chini ya ulinzi lakini watu wengine waliokuwa kwenye bodaboda walifanikiwa kutoroka," alifafanua.

Aidha, Kamanda Ngonyani alisema jeshi hilo linaendelea kuwatafuta watu hao pamoja na mtandao wa wafanyabiashara ambao wamekuwa wakijihusisha na ununuzi wa dawa za serikali kinyume cha sheria.

Kamanda Ngonyani alitaja dawa na vifaa tiba vilivyokamtwa kwa mtuhumiwa huyo kuwa ni vidonge vya uzazi wa mpango maboksi saba ambayo ndani yake kuna paketi 14 na vidonge aina ya Cipro maboksi 10.

Alitaja vifaa tiba vilivyokamatwa kuwa ni mabelo matatu ya vyandarua, mabunda mawili ya glovu zinazotumika katika upasuaji yakiwamo maboksi 10 ya glovu aina ya Latex na dawa zingine ambazo uchunguzi wake unaendelea.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila akizungumza na waandishi wa habari mkoni humo jana, kuhusu maandalizi ya mkutano mkubwa wa Kimataifa wa viongozi wa Afrika. Kulia ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Rehema Madenge. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkutano wakuu AU neema kwa Tanzania

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika (AU) utakaojadili kuhusu uwekezaji katika rasilimali watu, ni neema tele kwa Tanzania.

Amewataka Watanzania hususan wajasiriamali na wafanyabiashara kutumia fursa hiyo kukuza vipato vyao kupitia bidhaa na huduma watakazozitoa kwa washiriki. Mkutano huo wenye washiriki 1,200 ambao unatarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Julai 25, mwaka huu, Dar es Salaam.

Chalamila ametaka pia wananchi kuutumia kujenga taswira nzuri ya nchi ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameijenga kupitia hamasa kwenye sekta mbalimbali ikiwamo utalii.

Chalamila aliyasema hayo jana wakati akizungumzia kuhusu maandalizi ya mkutano huo utakaohudhuriwa na viongozi wakuu wa nchi za Afrika na mawaziri wa sekta za rasilimali watu. Hii ni mara ya kwanza mkutano huo kufanyika nchini na Afrika kwa ujumla.

Alisema agenda ya mkutano huo ni ukuaji wa uchumi imara kwa nchi za Afrika katika kuongeza tija kwa vijana kupitia kuboresha ujifunzaji na kukuza ujuzi. "Tanzania ni nchi ya mfano kwenye mambo mengi na imetumika tena kwa mara nyingine kuunda azimio la Dar es Salaam kuhusu rasilimali watu.

"Tunampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada na heshima kubwa ambazo ameendelea kujenga taswira njema ya nchi kwa nchi zingine za Afrika na zile za mabara mengine. Rais Samia amewekeza nguvu ya kubadili taswira ya nchi kimataifa na faida zake tumeanza kuziona kupitia mkutano huu mkubwa," alisema.

Chalamila alisema mkutano huo wa rasilimali watu bara la Afrika, uliofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ni moja ya sehemu ya utalii ambao Rais Samia amekuwa akihamasisha.

"Ujio wa mkutano huu ni muhimu kujenga utalii wa hoteli, fukwe na utalii wa vyakula. Wananchi wa Dar es Salaam tumieni fursa hii kukuza mapato na kukuza uchumi wa mkoa huu. Hoteli zaidi ya 40 zitatumiwa na wageni hivyo hii ni fursa ya utalii wa mkutano.

"Nia ya Mkoa huu ni kila mgeni anayekuja Dar es Salaam katika matumizi yake ya fedha anaacha dola ili nasi tuweze kunufaika katika kukuza uchumi, tumehamasisha wazalishaji na wajasiriamali mbalimbali wapatao 100 kushiriki maonyesho kwenye mkutano huo ili kuuza bidhaa zao zinazoonyesha uzalishaji, utamaduni na mila zetu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), kinachosimamia Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Balozi Ephraim Mafuru, alimpongeza Rais Samia kwa kufungua nchi na kuwezesha mikutano kama hiyo kufanyika nchini.

Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, akizungumzia kuhusu mkutano huo hivi karibuni, alisema miongoni mwa sababu za Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji ni kitendo chake cha kuimarika kwa amani na hatua ilizochukua katika kuwaendeleza vijana ikiwamo kuimarisha sekta za elimu na afya.

Pia alisema ni moja ya nchi za Afrika ambazo idadi ya watu inakua kwa kasi na ina hazina kubwa ya vijana.

# Rais aridhia hekta 18,000 kutolewa kwa wananchi

**Na Munir Shemweta,**
MULEBA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia kumegwa eneo la Ranchi ya Kagoma iliyoko katika wilaya za Muleba na Karagwe mkoani Kagera lenye ukubwa wa hekta 18,031 kwenda kwa wananchi kuendelea na shughuli mbalimbali za kibinadamu yakiwamo makazi.

Hayo yalibainishwa juzi katika kijiji cha Rutoro wilayani Muleba na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati wa kutoa mrejesho wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 kwa wananchi wa Rutoro.

Kutokana na kumegwa eneo hilo, wananchi wa Rutoro watakuwa wamepata asilimia 44.44 ya Ranchi ya Kagoma huku asilimia 55.56 ikibaki katika ranchi hiyo. Waziri Mabula alisema kitakachowatenganisha wawekezaji na wananchi baada ya uamuzi huo wa serikali ni mipaka mipya itakayowekwa

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, vijiji ambavyo wananchi wake watanufaika na uamuzi huo ni Rutoro, Kyobuheke, Mishambya na Byengeregere.

"Serikali haijafanya makosa kufanya maamuzi hayo bali ni utaratibu unaolenga kuwapunguzia adha waliyokuwa nayo wawekezaji kwa kugombana na wananchi na Mheshimiwa Rais hapendi hayo madhara yanayotokea kwa pande zote ndiyo maana uamuzi umechukuliwa kuwatenganisha," alisema Dk. Mabula.

Alisema utaratibu uliotumika kutoa maeneo kwa wananchi katika kata ya Rutoro utasaidia kumaliza tatizo la Mwisa II kwa kuzingatia mapendekezo ya mkoa wa Kagera.

Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, mbali na kupongeza uamuzi huo wa serikali, alionya wananchi wa Rutoro kuepuka kukaribisha watu baada ya uamuzi huo na kuwataka kutulia kuisubiri serikali iwapatie vitu walivyovikosa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliwataka wananchi kutovamia maeneo ya watu wengine hasa baada ya uamuzi huo na kueleza kuwa, kufanya hivyo ni kuingia katika hatia na serikali itachukua hatua kwa watakaofanya hivyo.

"Msivamie eneo la mtu yeyote hadi utaratibu utakapokuwa umekamilika na yaliyotangazwa hapa hayamfanyi mmoja kati yetu atoke aende kujimilikisha. Atakayefanya vitendo visivyo vya kiungwana kwa kuvamia eneo hatakuwa na mtetezi kutoka upande wowote," alisema Ulega.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Khamis Hamza Chilo, aliwataka wananchi wa Rutoro kuhakikisha wanapanda miti kwenye maeneo wanayoenda kuishi ili kutunza mazingira sambamba na kuondokana na athari ya tabianchi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera, Nazir Karamagi, alisema amefurahishwa na ziara ya mawaziri wa wizara za kisekta katika mkoa na kueleza kuwa ujumbe huo umekwenda na mamlaka kamili na kufanya uamuzi waliokubaliana kuhusiana na utatuzi wa mgogoro wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo.

Naye Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo, alisema anaamini baada ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kuwekwa kwenye eneo waliopatiwa wananchi na hatimaye wakulima kupangwa vizuri basi utaratibu wa miradi ya umwagiliaji utapelekwa na wakulima watanufaika na miradi hiyo.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABUBAKARY RAMADHANI LIBUHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CHASER** yenye usjaili namba: **T222 AQA,** CHASSIS NAMBA: **SX903018073** na ENGINE NAMBA: **4S123250.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/246234/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NDG.FABIAN K.NDOMBA.**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne (IV),chenye Index Na.**S.1715-0050,**kilichotolewa na Baraza la Mitihani-Taifa,kupitia shule ya secondari Shikula,iliyopo mkoa wa Songwe, mwaka 2019. Kwa yeyote atakayekiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

RIPOTI YA POLISI **MBE/MBE/RB/212811/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MIKESE, MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA.32/2023**
**MDAI: MBAMBA JAMES LONGIDO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: ALLY RAMADHAN MKASI**

**KWA: ALLY RAMADHAN MKASI**
**GWATA**

**OMBI LA MDAI: MBAMBA JAMES LONGIDO, MADAI YA PESA TSHS.1, 030,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika Shauri tajwa hapo juu bila kukosa,Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24 mwezi 7 mwaka 2023 saa2:30 Asubuhi.

**ANGALIA ALAMA:** kuhudhuria/Haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama imethibitisha kama umepokea/Mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/Mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 07 mwaka2023.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MIKESE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMWEL DAUDI MALECELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **OMARI HEMED AMIRI** namba za usajili **T272 DCT** aina ya **TOYOTA CARINA,** Chassis **No. AT2120100553.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi: **DOD/KON/RB/242400/2023**

RIPOTI MAALUM

# Matumizi ya gesi yalivyookoa mamilioni shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHULE imeachana na kuni, imegeukia matumizi ya gesi. Gharama za nishati shuleni zimeshuka kutoka Sh. milioni sita hadi Sh. milioni 3.3 kwa mwezi.

Ni mageuzi yanayoshuhudiwa sasa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ruvu wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Shule hiyo ni miongoni mwa taasisi za serikali zilizoitikia utekelezaji wa agizo la Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo la Aprili 19, mwaka huu la kuachana na matumizi ya kuni na makaa na kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya gesi ili kupunguza gharama na kulinda mazingira.

Mkuu wa Shule hiyo, Juliana Chimazi, amemwambia mwandishi wa habari hizi kuwa kwa muda mrefu kuni zimetumika shuleni kama nishati ya kupikia chakula cha wanafunzi.

Lakini Machi mwaka huu walifunga mtambo wa gesi wenye uzito wa Kg 1,000 kutoka kampuni ya Taifa Gas. Kwa wastani, kilo hizo 1,000 wanazitumia kwa siku 26, sawa na 38.46 kila siku.

"Tangu Aprili mwaka huu hatujaagiza kuni katika shule yetu. Tunatumia gesi kupikia vyakula vyote vya wanafunzi. Tumebaini kwa siku moja tunatumia Kg 38 za gesi.

"Kwa mwezi sasa tunatumia gharama ya Sh. milioni 3.3 kwa ajili ya gesi kulinganisha na awali ambapo tulikuwa tunatumia Sh. milioni sita kununua kuni," anabainisha.

Hii ina maana kwamba, shule hiyo sasa inaokoa Sh. milioni 2.7 kila mwezi. Kwa mwaka mzima itaokoa Sh. milioni 32.4. Zinatosha kujenga vyoo vya wanafunzi vyenye matundu 30. Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), tundu moja la choo cha wanafunzi linajengwa kwa Sh. 1,100,000.

Mwalimu Juliana anasema matumizi ya gesi pia yanaleta unafuu kwa kuandaa chakula cha wanafunzi kwa wakati tofauti na walipokuwa wanatumia kuni. Hawakuwa na uhakika wa muda wa chakula kuiva.

"Wakati tunatumia kuni kipindi cha mvua kuna muda chakula kilikuwa kinachelewa kidogo, kwani kuni nyingi zilikuwa mbichi na pia wakati mwingine magari yalikuwa yanakwama njiani na kuchelewa kufika kwa wakati," anaeleza.

Mwalimu Juliana pia anataja kikwazo kingine - kuni ambazo hazijakauka vizuri zilikuwa tatizo kwa wapishi kutokana na moshi mkali huku nyingine zikiwa nyepesi na kuisha haraka bila kuivisha chakula, japo suala hilo halikuathiri vipindi vya masomo kwa wanafunzi.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ruvu, Juliana Chimazi.

"Matumizi ya gesi yamekuwa mkombozi kwetu kwa kuokoa gharama za kununua kuni. Pia tumeokoa muda mwingi ambao ulitumika kusimamia uandaaji wa chakula cha wanafunzi kwa kutumia kuni," Mwalimu Juliana anasema.

Mwalimu wa Chakula shuleni huko, Japhet Daud, anasema kuna wakati kuni zilikuwa hazifikishwi kwa wakati shuleni.

Anataja mbinu waliyokuwa wanaitumia ili kutoathiri ratiba ya masomo shuleni, ni kuwa na akiba ya kuni waliyoweka wakati wa kuagiza mzigo mwingine.

Mbali na kuachana na matumizi ya kuni, katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, shuleni hiyo pia imewekeza katika kupanda miti kwa ajili ya kutunza mazingiara na kupata mbao.

Mwalimu wa Mazingira shuleni huko, Andrea Hadson, anabainisha kuwa mwaka 2022/23 walipanda miti 2,000 na kila mwaka wanajiwekea malengo ya upandaji miti.

"Mwaka 2021/22, zaidi ya miti 5,000 ilipandwa na kati ya hiyo, ni 400 pekee imeendelea kukua. Mwaka wa masomo uliopita (2022/23) ni miti 400 tu (kati ya 2,000 iliyopandwa), imebaki na tunaendelea kuitunza kwa sababu mingine hukauka kutokana na majanga ya moto pale wananchi wanaposafisha mashamba. Wanachoma moto ambao unaathiri miti yetu," anasema.

Mwalimu huyo anasema kuwa mbali ya moto, ukame, ardhi kuwa na udongo wa mfinyazi na mchwa, ni vikwazo vingine kwa ustawi wa miti wanayoipanda.

Anabainisha kuwa eneo la shule hiyo lina ukubwa wa ekari 154. Kati yake, ekari 70 zimepandwa miti huku zikiwa zinapakana na mashamba ya mpunga ya wanakijiji.

Kwa mujibu wa Hadson, mwaka huu wa masomo (2023/24), wanalenga kupanda miti 3,000 ya aina mbalimbali, ikiwamo ya mbao.

Mwalimu wa Miundombinu shuleni huko, Robert Israel, anasema miti ya mbao inayopandwa katika shule hiyo imekuwa inasaidia katika ukarabati wa majengo na madawati.

Anabainisha kuwa kwa mwaka 2018, walivuna miti minane ya mbao na mwaka huu miti mitatu imevunwa na kupata mbao 84 ambazo wametumia kufanya ukarabati.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, mbao moja inauzwa zaidi ya Sh. 6,000 na kwamba kupitia miti ya mbao waliyopanda na wanayoendelea kupanda, wanaokoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo na samani za shule.

Katika uzinduzi wa uzinduzi wa Kampeni ya Utunzaji Mazingira na Matumizi ya Nishati Mbadala Aprili 19 mwaka huu, Waziri Jafo alisema serikali inalenga matumizi ya gesi kufikia asilimia 80 ya Watanzania yote miaka 10 ijayo. Kwa sasa ni asilimia nane tu ya wananchi wanaotumia nishati hiyo.

Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Taifa Gas, Angel Bhoke, anasema kutokana na uharibifu wa mazingira unaochangiwa na ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa uliokithiri nchini, wameamua kuja na mpango wa kushindanisha halmashauri katika kupanda miti na kutunza mazingira.

Bhoke anasema kuwa gesi wanayouza ni safi na salama na haina moshi, hivyo kuwaomba wananchi waachane na matumizi ya kuni na mkaa, ambao ni hatari kwa afya zao.

Anasema kupitia matumizi ya gesi, wananchi wanaweza kuwa sehemu ya kupunguza ukataji wa miti ambao umekuwa ukiathiri vyanzo vya maji na umeme nchini.

"Tanzania tumekuwa tukipoteza ekari 400,000 za misitu kila mwaka. Hii inatokana na ukataji miti ambao athari zake tunaziona kwa vyanzo vya maji na kusababisha mgawo wa umeme nchini," anasema.

Hoja ya Bhoke kuhusu hatari za kiafya kwa watumiaji kuni na mkaa, inasadifu ufafanuzi wa Mtaalamu wa Magonjwa ya Upumuaji, Dk. Elisha Osati, anayesema kuwa kuni na mkaa hutoa chembe ndogo zinazoweza kupenya katika njia ya hewa, hata kusababisha athari kiafya.

Dk. Osati hewa chafu aina ya kaboni monoksaidi, inayotolewa na mkaa, pia kuni, inapoingia mwilini inapenya katika damu na kuanzisha athari ya kuondoa hewa ya oksijeni, ambayo ni muhimu kwa uhai wa mtu na ndio unakuwa mwanzo wa madhara ya muda mfupi na mrefu.

Mtaalamu huyo anabainisha madhara ya kuni na mkaa kwa mtumiaji yanajumuisha moyo kushindwa kufanya kazi, matatizo ya kupumua na hatimaye kupata maambukizi ya njia ya hewa (ARI), ugonjwa sugu wa mapafu (COPD), pumu, saratani ya mapafu au kwa wajawazito kujifungua watoto wenye uzito wa chini.

Shirika la Afya Duniani (WHO) tayari limeshaonya kupitia ripoti yake ya utafiti ya mwaka jana kwamba, moshi unaotokana na kuni za kupikia ni mojawapo ya visababishi vikuu vya vifo vya watoto wachanga duniani, ukigharimu maisha ya watoto 500,000 wenye umri chini ya miaka mitano kila mwaka.

Utafiti huo unachambua matumizi ya nishati hizo na kuenea kwa magonjwa ya kupumua kwa watoto hao kupitia utafiti uliofanywa katika nchi 30 zinazoendelea kutoka mabara ya Asia, Afrika na Amerika ya Kusini.

Matokeo yalipendekeza jamii kuweka nje majiko yanayotumia nishati hizo. Utafiti ulibaini watu bilioni tatu katika nchi zinazoendelea wanategemea kuni au mkaa kwa ajili ya kupikia.

Kwa mujibu wa WHO, magonjwa yanayosababishwa na moshi husababisha vifo vya watu milioni 4.3 kila mwaka, vikiyapiku magonjwa ya malaria na kifua kikuu (TB).

Mwishoni mwa mwaka jana (2022), Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika Mjadala wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia uliofanyika jijini Dar es Salaam, alielekeza kuwe na mpango mkakati wa miaka 10 ili kutumiza lengo la kitaifa la asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia gesi kupika katika mulongo mmoja ujao.

Juni mwaka huu, Waziri wa Nishati, January Makamba, aliliarifu Bunge kuwa tayari kumeshaundwa kikosi kazi husika kitaifa kinachojumuisha ngazi za wizara na taasisi zake, chini ya uratibu mkuu wa Wizara ya Nishati, huku kukiwapo kamati ya mawaziri inayoandaa dira, ambazo ni: Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Zingine ni: Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Afya, pamoja na wadau wa sekta binafsi, asasi zisizokuwa za kiserikali na washirikia wa maendeleo.

Kwa mujibu wa January, mkakati unatekelezwa mijini katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Pwani, Tanga na Tabora. Unafadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa thamani ya Euro milioni 30.

Waziri huyo alisema serikali kupitia Mradi wa Umeme Vijijini (REA), inaendelea kutekeleza programu inayowezesha kupatikana nishati safi ya kupikia na katika mchango wake, REA inawezesha usambazaji na kupatikana mitungi bora ya gesi kutoka sekta binafsi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alipozindua mtambo wa gesi wa kupikia katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ruvu wilayani Kibaya, mkoani Pwani, Aprili 19 mwaka huu. **PICHA: JULIETH MKIRERI**



Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Epson Luhwago (kulia) akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mwenza (Maendeleo ya Biashara) wa kampuni ya RedHorizons, Francisca Francis (katikati), kuhusu shughuli mbalimbali za uandaaji wa magazeti ya The Guardian na Nipashe yanayochapishwa na kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), alipotembelea ofisi za TGL, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja Operesheni wa RedHorizons, Twaha Kiduku na Mhariri wa Biashara wa TGL, Mnaku Mbani (aliyeketi). **PICHA: CARLOS BANDA**

# Mipango yawekwa kuimarisha usafiri Tanzania na DR Congo

**Na Scola Malinga,** KINSHASA

Waziri wa Fedha. Dk. Mwigulu Nchemba, amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ekila Libombo, kuhusu mipango ya kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kukuza biashara na uchumi wa nchi hizo mbili.

Mazunguzo hayo yalifanyika mjini Kinshara, DRC kando ya mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji wa jopo la mapitio ya uchumi mpana katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Katika mazungumzo yake, Dk. Nchemba alitaja maeneo kadhaa ya ushirikiano ikiwamo Tanzania kupatiwa kibali cha ndege za abiria za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kuanza kufanya safari kati ya mataifa hayo ili kuwezesha biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo.

"Ujenzi wa miundombinu ya barabara upande wa mashariki mwa DRC kuanzia maeneo ya jiji la Lubumbashi, Moba hadi Bandari ya Kalemie, na ujenzi wa reli ya SGR itakayounganisha nchi za Burundi na DRC kutokea Uvinza - Tanzania hadi Kindu, DRC kupitia Musongati na Gitega nchini Burundi ni miradi muhimu," alisema Dk. Nchemba.

Alisema maombi ya DRC ya kupatiwa eneo la bandari kavu kwa ajili ya kuhifadhia mizigo ya nchi hiyo linafanyiwa kazi na Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na taarifa itatolewa ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo kupitia bandari ya Dar es Salaam.

Dk. Nchemba pia alisisitiza umuhimu wa kuimarishwa kwa amani na usalama katika maeneo yenye mapigano hususan eneo la mashariki mwa DRC ili miundombinu inayotarajiwa kujengwa iwe na manufaa kwa watumiaji na hatimaye malengo yaliyokusudiwa ya kuimarisha biashara na huduma za usafiri kwa wananchi kufikiwa.

"Ni muhimu kupatikana amani eneo la mashariki mwa DRC ili kupitia ujenzi wa miundombinu inayokusudiwa kupita maeneo hayo ichochee uzalishaji mali na ufanyaji biashara na kukuza uchumi wa mataifa haya mawili," aliongeza.

Naye Likombo alisema nchi yake kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa anga inaendelea kufanya uchambuzi wa maombi ya ATCL la kufanyacbiashara nchini humo na taarifa za uamuzi utakaofikiwa itatolewa.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu ya barabara, Likombo alisema jitihada mbalimbali zinaendelea ili kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya barabara kuunganisha jiji la Lubumbashi na miji ya mashariki mwa DRC kama Moba na bandari ya Kalemie.

Alisema DRC imekubali kugharamia ujenzi wa kipande cha reli kutoka Uvira hadi Kindu na kwa sasa upembuzi yakinifu unafanyika ili kubaini gharama za ujenzi wa mradi huo. Alisisitiza kuwa ili miundombinu hiyo iwe na manufaa na kuruhusu ufanyaji biashara, suala la amani ya mashariki mwa DRC linapaswa kuwa ni la kipaumbele.

Likombo aliishukuru serikali ya Tanzania kwa kulifanyia kazi suala la kupatiwa eneo la Bandari kavu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya ufanisi wa usafirishaji wa mizigo kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda DRC na Tanzania kusaidia upatikanaji wa amani ya kudumu eneo la DRC mashariki ili miundombinu

# Wasichana 150 waokolewa kutoka biashara haramu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WASICHANA 150 wenye umri kati ya miaka 15 na 24 ambao walijifungua watoto na kuacha shule kisha kutelekezwa na wazazi wenzao, wameokolewa katika hatari ya kujiingiza katika biashara haramu.

Baada ya kuacha masomo na kutekelezwa, wasichana hao walijiingiza katika biashara ya ngono na ukahaba lakini sasa wameacha baada ya kupatiwa njia mbadala za kuendesha Maisha.

Wasichana hao kutoka katika kata za Bigwa, Mindu na Mzinga Manispaa ya Morogoro, wameanza kupatiwa mafunzo ya mradi wa Maua kwa Njia ya Digitali yanayotolewa na taasisi inayojihusisha na mifumo ya teknolojia ya Nexis Africa Limited kwa ufadhili wa Fedha za walipakodi wa serikali ya Uswisi.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi huo ulifanyika mkoani hapa, Mratibu wa Mradi unaofahamika kama Shamba Plusi kutoka Nexis Africa, Neema Shukuru, alisema mpango huo umelenga kuwasaidia kujiajiri au kuajiriwa kwa kutumia biashara ya kuuza maua na udongo kwa ajili ya bustani.

Alisema mpango huo wa mafunzo kupitia mradi wa Maua Kidigitali umekuja baada kufanya utafiti kwenye baadhi ya kata za Manispaa ya Morogoro na kubaini kuna kundi kubwa la wasichana waliozalishwa na kuacha masomo hatimaye kutelekezwa na wanaume zao wapo katika hatari ya kujingiza katika biashara hiyo isiyo rasmi kutokana na ugumu wa maisha na kuwa tgemezi kwa wazazi na walezi.

"Kabla ya kuleta mradi huu, tulifanya utafiti katika kata za Manispaa ya Morogoro na kubaini wapo wasichana waliokatishwa masomo kwa kupata watoto na wamekimbiwa au kutelekezwa na wazazi wenzao, hivyo wanapitia kwenye ugumu wa maisha na baadhi yao kujingiza katika biashara isiyo rasmi. Kutokana na hali hiyo , tukaona tuje na mradi huu wa kuwafundisha kilimo cha bustani ya maua na udongo ili wajikwamue kimaisha," alisema Shukuru,

Alisema kupitia mradi huo wasichana hao watafundishwa kwa nadharia na vitendo kupitia Kitalu Nyumba kitakachowekwa miundombinu ya kisasa ikiwamo ya umwagiliaji na mifumo ya upandaji wa maua katika kata hizo.

Ofisa kutoka katika mradi huo, Sitta Banzi, alisema serikali ya Uswisi kupitia mradi wake wa kuwajengea uwezo vijana kuondokana na umaskini unaofahamika kama SET, umelenga kuwasaidia wasichana hao kujikwamua kwa kufanya biashara zinazokubalika katika jamii ili kujipatia kipato na kuondokana na umasikini.

Alisema baada ya mafunzo hayo, wasichana hao wataunganishwa kwenye mfumo wa njia ya mawasilinao ya kidigitali kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali zikiwamo za kuendesha kilimo cha maua pamoja na masoko yaliyoko ndani na nje ya nchi.

Naye Dk. Rachel Zakayo, mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alisema soko la maua kwa sasa ni kubwa hasa ndani ya nchi kutokana na baadhi yake kutumika kama tiba mbadala na mengine mapambo kwenye myumba, hoteli kubwa na sehemu za starehe.

Alisema pamoja na kufundishwa kilimo cha maua, kundi hilo litajifunza pia namna ya kutumia udongo kwa ajili ya kuanzisha bustani za maua na kwa sasa mahitaji ya soko yamekuwa makubwa kutokana na ujenzi wa nyumba za

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera CECAFA kuendeleza vipaji wachezaji wanawake

**BARAZA** la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), limetangaza mashindano ya wasichana wa umri chini ya miaka 18 yatafanyika kuanzia Julai 25 hadi Agosti 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mashindano hayo mwaka huu yatafanyika kwa kushirikisha nchi sita wanachama kati ya mataifa 12, yanayounda baraza hilo kongwe hapa barani Afrika.

Nchi zitakazoshiriki ni pamoja na wenyeji Tanzania Bara, Uganda, Ethiopia, Burundi na Zanzibar ambayo katika CECAFA ni mwanachama kamili wakati ambao hawataleta timu ni Kenya, Sudan, Sudan Kusini, Djibouti, Eritrea, Somalia na Rwanda.

Wenyeji Tanzania Bara watakutana na Burundi katika mechi ya ufunguzi wakati mapema siku hiyo Ethiopia itawakaribisha Uganda.

Katika miaka ya nyuma, CECAFA ilikuwa maarufu sana ikiandaa vyema mashindano yake ya mabingwa wa nchi ambayo maarufu yalijulikana kwa jina la Kombe la Kagame (Kagame Cup), hii ilitokana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kudhamini michuano hiyo kwa muda mrefu.

Kagame Cup ilikuwa ndio 'brand' kubwa ya CECAFA kwa kipindi kirefu ikifuatiwa na mashindano ya Kombe la Chalenji ambayo yalishirikisha timu za taifa za wanaume.

Mashindano haya yalipoteza umaarufu wake kutokana na ratiba na kalenda za mashindano ya kimataifa kubadilika. Miaka ya hivi karibuni, klabu zilitaka kutumia muda ambao michuano hiyo hufanyika, kwenda ughaibuni kufanya maandalizi ya msimu mpya na matokeo yake baadhi ya timu zilijiondoa na kupoteza mvuto wake.

Baada ya sintofahamu hizo, CECAFA imeamua kuwekeza nguvu zake katika mashindano ya vijana na hasa yanayohusu soka la wanawake. Kila mwaka tumeshuhudia michuano ya kuanzia umri wa miaka 17, U-20 na sasa tunaelekea kuzindua mashindano ya U-18.

Tunapenda kuipongeza CECAFA kwa kuendesha na kusimamia mashindano haya ya wasichana na tayari matunda yake yalionekana mwaka jana kwa ukanda huu kupata mwakilishi aliyeshiriki fainali za Kombe la Dunia kwa wasichana za umri chini ya miaka 17, naye ni timu ya Tanzania (Serengeti Girls).

Pia mafanikio ya Simba Queens iliyofika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake hapo mwaka jana yalichangiwa na uwepo wa michuano ya ngazi mbalimbali inayofanyika kwende ukanda huu, mafanikio kamwe hayapatikani kwa miujiza, bali kwa wachezaji kuandaliwa vyema.

Hata hivyo, ni jambo la kushangaza kwa nchi ambazo zimeshindwa kuwaandaa wachezaji wake na kushiriki mashindano hayo, ambayo yalitajwa mapema mwaka huu katika kalenda iliyotolewa na CECAFA.

Kupitia mashindano haya, wachezaji wasichana wanapata nafasi ya kupata uzoefu wa kushiriki mashindano ya kimataifa na pale wanapoitwa katika timu za taifa, wanakuwa wameimarika na wako tayari kushindana.

Tunawakumbusha wadau na viongozi wa soka wa nchi kutoka CECAFA na nyinginezo, kutumia vyema fursa hizi za kushiriki mashindano ya vijana, kwa sababu ndio sehemu pekee wachezaji wanapata uzoefu.

Ni jambo lisilojificha, nchi nyingi zimekuwa na changamoto ya kuendesha ligi au mashindano mbalimbali ya klabu yanayohusisha timu za wasichana, sasa inapotokea nafasi kama hii, ni vyema nchi zisijitoe, ziwape nafasi wachezaji chipukizi wasichana kuonyesha vipaji vyao.

Mashindano ndio sehemu sahihi kila kocha hufahamu uwezo wa wachezaji wake, na baada ya kumaliza hurejea kufanya tathmini itakayomsaidia katika kuimarisha kikosi chake lakini kuongeza nyota kwenye timu ya wakubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Skudu wa Yanga 'somo' kwa wachezaji wasidanganye umri

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** mwingine huwezi kujua mashabiki wa soka wa hapa nchini wanataka nini, kati ya umri au uwezo wa mchezaji.

Huwezi kujua wanataka kuongopewa au kuambiwa ukweli kuhusiana na umri wa mchezaji aliyesajiliwa na timu yao kwa sababu, wakidanganywa mara nyingi huamini na wakiambiwa ukweli hawataki.

Yanga imemsajili mchezaji mpya kutoka Afrika Kusini, Mahlatse Makudubela ambaye wenyewe wanamwita 'Skudu Master' kutokana na uwezo wake mkubwa wa kucheza soka na kuuchezea vyema mpira.

Mchezaji huyo amesema ana umri wa miaka 33. Nasema ametuambia kwa sababu yeye mwenyewe ndiye aliyetamka hivyo.

Hajaamua kudanganya watu, hasa mashabiki wa soka Tanzania na Afrika nzima kuwa ana umri chini ya huo.

Anachoangalia yeye ni soka lake mguuni, hivyo haoni shida kuwaambia wana ana umri huo.

Ni umri ambao kwa Tanzania wengi wanadai mchezaji mwenye umri huo ni mzee na anacheza soka la kubahatisha, hasa kwenye timu kubwa.

Mashabiki wa soka Bongo hawaelewiki nini wanataka. Kwa sababu unaweza kusajili mchezaji mwenye umri mdogo wanayemtaka wao lakini kiwango chake kikawa duni, huku pia unaweza kukuta umenasa nyota mwenye umri mkubwa lakini hamna kitu.

Klabu siku zote hazitaki umri wa mtu, zinataka uwezo wake uwanjani na si umri wake.

Mfano mdogo hapa kwetu ni nahodha wa Simba, John Bocco, ana umri mkubwa kuliko mastraika wengi vijana wa Kitanzania, lakini ndiye ana mabao mengi zaidi kuliko hao wenye umri mdogo.

Ndiyo maana Simba hawajamwacha, kwa sababu kama wakifanya hivyo, straika yupi Mtanzania mwenye rekodi kama yake, ili wakimwacha Bocco wakamchukue?

Hakuna, ndiyo maana wamebaki naye na anaweza pia akaendelea kuwashangaza wengi katika msimu ujao wa 2023/2024.

Kwa jinsi alivyo mwepesi, uwezo wake na hata mwonekano wake, Makudubela angetuambia ana miaka 23, hakuna mtu ambaye angepinga.

Angeonekana kijana na kumwita majina mengi ya ujana, lakini yeye mwenyewe ameelekeza zaidi katika kuonyesha kipaji chake zaidi kuliko kudanganya umri.

Tumeona hata kwenye ligi ya vijana chini ya miaka 20, baadhi ya wachezaji hata kwa kuwaangalia hawakuwa na umri uliokuwa unatakiwa ili kushiriki michuano hiyo, lakini walicheza na walitambulika hivyo.

Walionekana ni wakubwa zaidi ya miaka 20, lakini wametudanganya ni vijana na tumekubali, ingawa baadhi ya watu ambao hawadanganyi kwa urahisi wanaguna pembeni.

Ukiangalia hata kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara wapo baadhi ya wachezaji ni wakubwa sana kuliko hata Skudu, kwa sababu wanacheza ligi kwa zaidi ya miaka 10, wanahama timu hii kwenda hii lakini wanadai bado ni vijana kitu ambacho si kweli.

Umri anaoutaja Skudu wachezaji kibao wa Ligi Kuu wana umri huo, lakini kwenye mitandao ya kijamii wamekuwa wakimwita mzee kwa sababu tu amekuwa mkweli.

Kama umri huo ni wa wazee, basi tuna wazee wengi sana kwenye ligi zetu hapa bongo.

Kama kwenye ligi ya vijana kuna wachezaji wenye zaidi ya miaka 20 na wanajiita U-20, jiulize kwenye Ligi Kuu tuna wachezaji wangapi 'vibabu'.

Ifike mahali mashabiki wa soka nchini wamjaji mchezaji kwa kiwango chake na si umri wake, kwa sababu hata wachezaji wa nje waliokuja hapa kama, Ismael Sawadogo walikuwa na umri mdogo lakini viwango vyao vilikuwa vidogo.

# Simbachawene ahimiza wananchi kuibua miradi

**Na Lusungu Helela,** KIBAKWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka wananchi kuibua miradi ya kimkakati katika maeneo yao ili Serikali iwasaidie kuikamilisha.

Simbachawene alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti katika Kata za Luhundwa, Lufu, Wangi na Wotta, Mpwapwa mkoani Dodoma kupitia mikutano ya hadhara.

Mikutano hiyo ya Waziri Simbachawene ni ni mwendelezo wa ziara katika jimbo la Kibakwe kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema serikali inavutiwa na uongozi wenye maono na mtazamo wa kimapinduzi kwa kuanza kusaidia pale nguvu za wananchi zilipoishia ili kuistawisha jamii hiyo.

Alitolea mfano wa miradi hiyo ya kimkakati kuwa ni ujenzi wa shule, zahanati, nyumba za watumishi na ujenzi wa kumbi za mikutano.

"Viongozi na watendaji mna kazi kubwa ya kuhakikisha wananchi wanashiriki katika ujenzi wa miradi ya maendeleo kwani wenye uhitaji ni sisi. Hatutegemei kuona nyie mko nyuma katika kutekeleza miradi hiyo. Kila mmoja ana wajibu wa kuchangia na kuona miradi inakamilika kwa wakati na kusimamia matumizi ya fedha zilizotolewa na serikali," alisisitiza.

Alisema serikali ina vipaumbele vingi, hivyo nguvu za wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo haiepukiki.

Simbachawene aliongeza kuwa jamii inayojitegemea hujipatia heshima, hivyo kitendo cha vijiji hivyo kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo yake kunaleta heshima kwa viongozi na wananchi kwa ujumla.

Kutokana na hali hiyo, Simbachawene alipongeza jitihada za viongozi na watendaji wa kata za Wangi na Wotta kwa kubuni miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa zahanati na ofisi za mwenyekiti wa kijiji, kisha kuiomba serikali isaidie kukamilisha kazi hiyo.

"Wananchi mkileta ndoo ya maji au mchanga inahesabika mmechangia, mchango sio lazima fedha," amesisitiza.

Amesema serikali itaendelea kusaidia kukamilisha kwa haraka miradi iliyobuniwa na wananchi kwani kwa kufanya hivyo kutachochea ushindani wa maendeleo katika jamii.

Katika hatua nyingine, Simbachawene alitoa wito kwa viongozi wa kata zingine kubuni na kutekeleza miradi kwa kutumia nguvu za wananchi katika maeneo yao ili kuichochea Serikali kuwaongezea nguvu katika hatua za ukamilishaji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, George Fuime, alisema wataangalia uwezekano wa kutenga fedha za kumalizia ujenzi wa ofisi ya mwenyekiti wa kijiji cha Lwihomelo kwa nia ya kuunga mkono shughuli zinazofanywa na wananchi wa Kijiji hicho.

"Mheshimiwa Waziri tutajitahidi katika kuhakikisha fedha zinatengwa kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za wananchi katika masuala ya maendeleo yaliyobuniwa na wananchi wenyewe, alisema Fuime.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja (katikati), akipata maelezo ya mradi wa maji wa Masanga-Ndolele-ji, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga jana ambapo alielezea kuridhishwa na maendeleo ya mradi huo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mamlaka yataja mikakati kukabili upotevu maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda (BUWSSA), imetaja mikakati ya kukabiliana na upotevu wa maji, ikiwamo kuondoa mita 6,000 zilizokaa zaidi ya miaka 10.

Aidha, mamlaka hiyo imeandaa andiko la mradi kwa ajili ya kukopa Sh. Milioni 815 kutoka mfuko wa maji, ili kuhakikisha upotevu wa maji unapungua kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mkurugenzi Mtendaji wa BUWSSA, Esther Gilyoma, alisema hayo juzi juzi jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi na mwelekeo wa kufikia asilimia 95 ya huduma ya maji mjini Bunda ifikapo mwaka 2025.

Alisema upotevu wa maji hasa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulikuwa asilimia 36 na kwamba mamlaka imeweka mikakati ya kupunguza tatizo hilo ikiwamo mpango wa miaka mitatu ulioanza mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2023/24 unaoendana na mpango wa kibiashara wa mamlaka ya maji.

Alifafanua kuwa fedha hizo zitakazokopwa zitawezesha kudhibiti upotevu wa maji kutoka asilimia 36 sasa hadi asilimia 15.

"Mamlaka hii ina chujio la kutibu maji eneo la Nyabehu ambapo maji yamekuwa yakitibiwa na kwa sasa Mamlaka haina huduma ya majitaka. Magari ya watu binafsi ambayo yanasimamiwa na Halmashauri ya Mji wa Bunda ndiyo yanatumika katika kutoa huduma za majitaka,"alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka huu wa fedha, wataanza kujenga miundombinu ya majitaka eneo la Butakale liliyoko Mjini Bunda.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mamlaka ina jumla ya wateja 7,556 kati ya hao, ni wateja wa majumbani, taasisi na biashara.

# Vijana 1,000 wafadhiliwa elimu ufundi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukuza ujuzi kwa vijana, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeingia makubaliano na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kufadhili wanafunzi 1,000 wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (VETA).

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, alisema benki hiyo imekuja na mpango wa kukuza ujuzi ambao utasaidia mkakati wa Serikali katika kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Alisema ufadhili huo unakwenda kutimiza azma ya serikali ya kutoa elimu na mafunzo yatakayo wawezesha vijana wa kitanzania kupata ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa.

Prof. Mkenda alisema NBC itatengeneza mfumo wa uwazi wa matumizi ya fedha hizo ili kutoa matokeo yaliyokusudiwa katika kuwajengea ujuzi vijana kujitegemea badala ya kusubiri kuajiriwa pekee.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema benki hiyo itatoa kiasi cha sh.milioni 100 kwa ajili ya kufadhili vijana 1000 watakaokwenda kusomea kozi katika vyuo mbalimbali vya VETA nchini. "Mpango huu unaitwa 'NBC Wajibika Scholarship'. Tunatambua tatizo la ajira kwa vijana na ni kilio cha dunia nzima. Kupitia mpango huu, tutatoa ufadhili kwa vijana 1,000 na huu ni mwanzo tu idadi itakuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka tunaamini hawa wakiweza kujiajiri tutakuwa tumepunguza kwa kiasi Fulani," alisema Sabi.

Alitaja baadhi ya kozi zitakazofadhiliwa kuwa ni ushonaji, uselemara, ufundi wa magari, ufundi ujenzi, upambaji na kozi nyingine watakazobaini zina fursa nyingi kwa vijana kujiajiri. " Mbali na ufadhili huu, benki itawaingiza vijana hao kwenye mpango maalumu wa elimu ya fedha ujulikanao kama NBC Business Club na tutaweza kuwafungulia akaunti maalumu zijulikanazo kama NBC kuwa nasi zisizokuwa na makato yoyote ili wajiwekee akiba," alisema.

Alibainisha kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, NBC imewekeza Sh. milioni 350 katika kutoa ufadhili wa vijana 70 wa ngazi za elimu ya juu na imekuwa ikishiriki katika ujenzi na ukarabati wa miondombinu ya shule mbalimbali hapa nchini.



Mtoto Yusra Gaza akiwa amebebwa na mama yake mzazi, Madawa Ally katika kijiji cha Kwasemwaliko, kata ya Kilulu, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi, ambapo anaomba msaada wa fedha kwa wasamaria wema ili aweze kutibiwa matatizo ya moyo wake mkubwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). Kutoka (kushoto) ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwasemwaliko, Madunda Hassani, baba mzazi wa mtoto huyo, Omari Gaza na Mwenyekiti wa kitongoji cha Bagamoyo, Mwantumu Msenga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mradi bil. 10/- kumaliza tatizo la maji

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), inatekeleza mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 10 katika eneo la Kisewe, Kata ya Chamazi Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam.

Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Lilian Masilago, alisema jana kuwa mradi huo ni mwendelezo wa juhudi za mamlaka kuhakikisha inafikisha huduma ya maji katika eneo lake la kihuduma kupitia miradi mbalimbali.

Alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya Kassco/Ceytun ambapo jana, kulifanyika kusafisha mabomba kwa kupitisha maji kwa msukumo mkubwa pamoja na kutoa upepo katika matoleo maalumu ya kutolea upepo katika eneo la Kisewe.

Mhandisi Masilago alisema hatua hiyo imelenga kufikisha huduma ya maji katika eneo la Kisewe ambalo kwa mara ya kwanza linapata maji ya bomba kwa kuwa awali, huduma ya maji ilikuwa ni ya kupitia visima vya jamii.

Alisema kazi hiyo ya kusafisha mabomba imefanyika kwa masaa manane ili kuhakikisha mabomba yanakuwa safi na huduma ya maji inafika maeneo hayo kwa kuzingatia ubora na viwango kwa mujibu wa usanifu uliofanywa.

Mradi huo wa uboreshaji wa huduma ya majisafi pembezoni mwa mji umetekelezwa kwa Sh. bilioni 10 ambapo unahudumia wananchi wa maeneo ya Temeke na Ilala. Alisema wananchi hao watapatiwa huduma kutoka kwenye chanzo ambacho ni tenki la mradi wa maji Kibamba-Kisarawe lenye ujazo wa lita milioni sita.

Pia alisema mradi huo unahusisha usambazaji wa maji katika Wilaya ya Kigamboni ambapo chanzo cha maji ni visima virefu vya Kigamboni.

Katika hatua nyingine, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja, ametembelea na kukagua mradi wa maji wa Masanga-Ndoleleji, Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga na kuridhishwa na maendeleo ya mradi huo.

Mhandisi Luhemeja alisisitiza kuwa pamoja na kazi kwenda vizuri ni muhimu kwa mkandarasi kumaliza kazi hiyo kwa wakati ili wananchi wapate maji kwa haraka.

"Nimeridhishwa na ubora wa miradi ya maji wilayani Kishapu, kazi inakwenda vizuri na mwaka huu mpya wa fedha, watapokea Sh. bilioni saba kutekeleza miradi ya maji," alisema.

Mhandisi Luhemeja aliagiza wataalamu wa wizara hiyo wanaosimamia mradi huo, kuhakikisha maji ya Ziwa Victoria yanafika na kusambazwa kwa wananchi kupitia mradi huo kwa sababu ni chanzo endelevu.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, aliishukuru serikali kwa kuleta fedha za miradi ya maji eneo hilo na kupongeza hatua za wizara kutumia maji ya Ziwa Victoria kama chanzo cha kuaminika zaidi katika mradi.

Mhandisi Valeriana Tovagonze kutoka Kampuni ya Mponela Construction & Co Ltd wanaotekeleza mradi huo, alisema kazi hiyo imefikia asilimia 75 na ifikapo mwezi ujao, wananchi wataanza kupata huduma.

Mradi wa maji Masanga-Ndoleleji unagharimu Sh. bilioni 1.6 na umehusisha ujenzi wa matenki mawili yenye ujazo wa lita 100,000 kila moja na utahudumia wakazi zaidi ya 12,700 pindi utakapokamilika.

# Mikoa vinara uchomaji misitu yatajwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MIKOA mitatu nchini imebainika kuongoza katika uchomaji moto misitu kutokana na kukithiri kwa shughuli za kilimo, ufugaji na urinaji asali.

Hatua hiyo imesababisha kupotea kwa zaidi ya kilometa za mraba 95,700 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya misitu ya Tanzania nzima.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) Dk. Revocatus Mushumbusi, aliiambia Nipashe juzi kuwa takwimu hizo ni za mwaka 2021/22 wakati taasisi hiyo ilipoamua kufanya utafiti juu ya moto na athari zake kwenye misitu.

Dk. Mushumbusi aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Tabora, Katavi na Lindi. Kutokana na kukithiri kwa jambo hilo, aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuacha kuchoma moto ovyo na kuzingatia elimu wanayopewa kuhusu athari zinazopatikana kwa kuanzisha moto usio wa lazima. "Ni muhimu kutoa tahadhari ya viashiria vya moto vinapoonekana na kutoa tahadhari kwa watu walioko saiti. Hii itasaidia na wao kufanya utaratibu wa kuuzima mapema na kuepusha na athari za uharibifu wa mazingira sambamba na misitu ambayo ni rasilimali adhimu nchini, " alisema.

Dk. Mushumbusi alisema moto huathiri uwekezaji katika sekta ya misitu na hata mtu akiwekeza kwa muda mrefu kwa pesa nyingi anaweza kupoteza vyote, hivyo akawataka wakulima, wafugaji na wanaorina asali kuacha mara moja matumizi ya moto katika kuandaa mashamba, maeneo ya malisho na kuvuna asali kwa sababu moto huleta athari kubwa za kijamii na kiuchumi kufuatia kugusa maslahi ya nchi. Mmoja wa wadau wa mazingira mkoani Morogoro, Deogratius Ignas, alikeme tabia ya baadhi ya wakulima kuandaa maeneo ya kilimo pamoja na kutafuta mashamba kwa kuchoma moto misitu kitendo ambacho kinaathiri mazingira.

Ignas ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la AgriWezesha mkoani Morogoro, aliwashauri wakulima na wafugaji kutumia mbinu bora za kupata ardhi ya kilimo na malisho kwa kuandaa maeneo bila kuathiri misitu.

# Waomba msaada matibabu mtoto

**Na Steven William,** MUHEZA

WAZAZI wa mtoto mwenye umri wa mwaka moja na miezi mitatu, mkazi wa kijiji cha Kwasemwaliko, Muheza, Tanga (pichani) aliyezaliwa na tatizo la moyo mkubwa, wanaomba wasamaria kumsaidia apate matibabu.

Akizungumza na mwandishi wa Habari hii juzi, mama mzazi wa mtoto huyo, Mwadawa Ally, alisema anaomba msaada kwa wasamaria ili mtoto wao aende Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa matibabu kutokana na kuwa na kipato duni.

Alisema mtoto wake alikuwa akisumbuliwa na kifua kwa kukohoa mara kwa mara ndipo alipompeleka katika Hospitali ya Teule Wilaya ya Muheza kupatiwa matibabu lakini bado tatizo hilo liliendelea mpaka alipompeleka Hospitali ya Siha jijini Tanga na kugundulika kuwa na tatizo la moyo mkubwa.

"Nimerudi nyumbani kijijini, sijui cha kufanya kwa kuwa hali yangu ya kimaisha ni duni. Sina fedha za kumpeleka Muhimbili. Ninaomba msaada kwa wasamaria wema kumsaidia mtoto wangu ili apate matibabu," alisema.

Alisema baadhi ya watu walimwambia akate bima ya Sh. 432,000 lakini kutokana na changamoto ya maisha hana fedha hizo.

Mama huyo alisema jitihada ambazo amezifanya ni kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwasemwaliko Madunda Hassan, kumwomba kibali cha kuchangisha fedha ili kumpeleka mtoto wake hospitalini.

Mwenyekiti wa Kijiji, Hassan na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bagamoyo, Mwantumu Msenga, kwa nyakati tofauti walisema wamepata taarifa za mtoto huyo na tayari wameshamwandikia barua ili kuomba msaada kwa mbunge na mkuu wa wilaya hiyo.

Baba mzazi, Omari Gaza, alisema mtoto wao amekuwa akikohoa hasa usiku na kukosa usingizi na kuomba wasamaria wema kusaidia kupata fedha za matibabu.

Wazazi hao wameomba kwa yeyote atakayeguswa na tatizo la mtoto wao wawasiliane nao kwa namba 0719207999 au 0693592987.



## HABARI DODOMA

# Magonjwa yasiyoambukiza Yazidi kuongezeka

**Na Gloria Maganza,** OUT

IMEELEZWA kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza hasa shinikizo la juu la damu, sukari na mfumo wa hewa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, mwaka huu.

Kutokana na hali hiyo, serikali inatarajia kufanya utafiti wa kitaifa utakaobaini hali halisi ya mwenendo wa viashiria hatarishi na magonjwa hayo Agosti, mwaka huu, kwenye mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar.

Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa Utafiti wa Kitaifa wa Viashiria vya Magonjwa Yasiyoambukiza (Steps Survey 2023) jijini Dodoma. Alisema takwimu zilizopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini zinaonyesha kwamba kumekuwa na wagonjwa 1,456,881 wa shinikizo la juu la damu sawa na asilimia 49 kulinganisha na asilimia 34 kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

"Kisukari wagonjwa 713,057 sawa na asilimia 24, magonjwa ya mfumo wa hewa wagonjwa 386,018 sawa na asilimia 13 ikilinganishwa na asilimia 10 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22,"alisema.

Mazrui alisema, takwimu zinaonyesha kuwa magonjwa hayo yameongezeka mara tano hadi tisa zaidi kati ya miaka ya 1980 ambayo asilimia moja ya Watanzania walikuwa na tatizo la kisukari na asilimia tano walikuwa na tatizo la shinikizo la juu la damu wakati kwa sasa tatizo la kisukari limefikia asilimia tisa na shinikizo la juu la damu limeongezeka na kufikia asilimia 25.

Aidha, alisema magonjwa hayo yasiyoambukiza yanachangia takribani asilimia 33 ya vifo vyote nchini.

"Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa mwaka 2020 zinaonyesha kuwa magonjwa haya yalichangia zaidi ya vifo milioni 41 sawa na asilimia 71 ya vifo vyote duniani kulinganisha na vifo milioni 57 kwa mwaka 2016 duniani," alisema.

Pia alisema katika kukabiliana na ongezeko la magonjwa hayo, serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na magonjwa hayo nchini kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna bora ya kujikinga na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya kwa kufikisha huduma za uchunguzi wa awali na matibabu kuanzia ngazi ya afya ya msingi.

"Kufuatia mwenendo na hali ya magonjwa haya nchini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na WHO itafanya utafiti wa kitaifa utakaobaini hali halisi ya mwenendo wa viashiria hatarishi na magonjwa yasiyoambukiza.

"Utafiti huu utakuwa ni wa pili baada ya ule wa kwanza uliofanyika mwaka 2011 upande wa Zanzibar na mwaka 2012 kwa upande wa Tanzania Bara,"alisema.

Mazrui alisema utafiti utahusisha watu wenye umri kati ya miaka 18 hadi 69 na unapaswa kufanyika kila baada ya miaka minne hadi mitano.

"Utafiti huu ni muhimu sana hasa katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza na takwimu hizo za kisayansi zitaonesha juu ya ukubwa wa viashiria vya magonjwa hayo nchini ambavyo vinaweza kutumika katika kuandaa mikakati ya kudhibiti magonjwa hayo nchini," alisema.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema magonjwa hayo kwa sasa yamekuwa yakiongezeka kwa kasi na kuongeza mzigo mkubwa wa bajeti ya serikali hususani Wizara ya Afya na gharama kwa familia.

Prof. Nagu alisema utafiti huo utasaidia kujua ukubwa wa tatizo na kuwawezesha kujipanga katika kugawa rasilimali kwa kuwa watakuwa wanajua tatizo, hivyo kutambua tatizo lilipo na kutibu mapema.




Kaimu Meneja wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mhandisi Rashid Kalimbaga, akisoma taarifa yake kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Ludovick Nduhiye (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa kikao cha faragha cha bodi hiyo, mkoani Singida juzi. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Canada yamwaga mabilioni kusaidia mapambano mimba, ndoa za utotoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na mkoa wa Tabora kukabiliwa na ukatili wa kijinsia, ndoa na mimba za utotoni, Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) limetoa msaada wa Dola za Canada milioni 15 ili kuondoa vikwazo hivyo na kuboresha maisha ya wasichana.

Akizungumza juzi baada ya Waziri anayehusika na Maendeleo ya Kimataifa na mwenye dhamana ya Shirika la Maendelo ya Uchumi nchini humo, Harjit Sajjan kutangaza msaada huo, Mkurugenzi wa Mradi wa BRIGHT kutoka Shirika la Nutrition International, Raphael Maligo, alisema mradi huo utatekelezwa kwenye wilaya zote za mkoa huo.

"Takwimu za serikali zinaonyesha vijana wanaopewa mimba chini ya umri wa miaka 15 ni asilimia 43 na asilimia 58 ya vijana wanaolewa mapema kwenye ukatili wa kijinsia Tabora ina asilimia 71," alisema.

Alisema mradi huo unawalenga vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 19 walioko shuleni na nje ya shule.

"Lengo ni kuhakikisha vijana balehe wanapata elimu ya afya ya uzazi na lishe kwa kutoa huduma jumuishi pamoja na afya ya uzazi. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya vijana walio kwenye umri wa balehe kupata mimba bila kupangilia.

"Mradi unalenga kuondoa changamoto hizo kwa kufanya vijana walioko kwenye umri balehe wapate huduma kamilifu na waendelee kuwa na afya njema," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mradi utahakikisha vijana hao wanakamilisha mzunguko wao wa shule na kuwa na matokeo mazuri.

# CCK yaonya malumbano kuhusu uwekezaji bandari

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Kijamii (CCK) kimetahadharisha kuwa malumbano yanayoendelea kuhusu uwekezaji wa bandari ya Dar es Salaam hayana afya na yanaligawa taifa na hivyo kimeitaka serikali na wadau wengine kufikia muafaka.

Katibu Mkuu wa CCK, Renatus Muabhi, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema ili kufikia mwafaka wa suala hilo kuna haja ya kuandaa mdahalo wa kitaifa ili kutathimini msimamo wa serikali na maoni ya wananchi.

Muabhi alisema njia nyingine ya kufikia tamati suala hilo ni kuunda tume huru ya wadau itakayoshirikisha wajumbe kutoka makundi tofauti yenye mawazo huru, kukusanya maoni na kutathimini msimamo wa wananchi, jambo ambalo litaleta muafaka na maridhiano kwa makundi yote yanayokinzana.

"Kikatiba mamlaka ya nchi yapo chini ya wananchi, tutafute na tuelewe maoni ya wananchi yanataka nini na hofu yao ni nini, hofu na mashaka yao vikiondolewa kwa kuridhiwa, tuanze utekelezaji wa uwekezaji kwa kuwa hofu na mashaka vitakuwa vimetibika kwa mamlaka ya wananchi wenyewe," alisema.

Muabhi aliongeza kuwa tusiruhusu kelele uchwara za wachache wenye hila zao binafsi, kutaka kuburuza umma kwa tamaa zao za mali jambo ambalo halitasaidia kumaliza mvutano huo. Alisema viongozi lazima watambue kuwa Serikali iliyopo madarakani ni ya watu, iliwekwa na watu kwa ajili ya watu na wanaipenda hivyo wanayo mamlaka kisheria kuikosoa bila kutishwa.

"Niwakati wa maridhiano, tukiri umoja wetu umetikiswa, imani ya wananchi kwa serikali yao imetoweka, michuano hii ya hoja inakoleza maswali kwa wananchi wasiojua mambo ya siasa na mikataba, ni wakati wa maridhiano," alisema.





## SMZ yatia saini utafiti wa madini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kutambua aina za madini yaliyoko, serikali imetiliana saini hati za ushirikiano na kampuni ya Aseel Oilfield Services Limited ili kufanya utafiti wa kutambua Zanzibar ina madini ya aina gani.

Akizungumza jana katika hafla ya kutia saini makubaliano hayo iliyofanyika mjini Zanzibar, Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Shaibu Kaduara, alisema ushirikiano huo utatimiza ndoto za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, za kuweka wizara hiyo inayohusu madini.

Alisema wizara hiyo ni moja ya taasisi za umma inayotegemewa na serikali na wananchi wake na inagusa maisha ya wananchi kila siku.

Kaduara alisema wako watakaobeza mambo hayo lakini kazi kubwa inayofanywa kupitia taasisi zake ni kuona Zanzibar inainuka kimaendeleo.

"Ushirikiano wetu ndio unaotoa uhai ya wizara hii ambayo ndiyo inayotoa uhai wa huduma za jamii. Haikuwa rahisi kwa yeyote anayesikia kwamba Zanzibar ina wizara inayohusu madini na wako wanaoniuliza Zanzibar kuna madini kweli sasa watapa jibu kwani ni nchi na tuna bahari," alisema.

Aliwaomba wananchi na taasisi mbalimbali kushirikiana na kuwa tayari katika mambo ya kimaendeleo na dunia ilipofikia ni lazima kupata watu wa aina hiyo na kushirikiana nao kupata njenzo ambazo zitasaidia kupiga hatua kubwa kupitia sekta mbalimbali.

Pia aliiomba kampuni hiyo kutobakisha malengo yao ndani ya makaratasi na badala yake kuyafanyia kazi kama ilivyokusudiwa na kutoa tija kwa nchi.

Aliahidi kuwa wizara itatoa kila aina ya ushirikiano kuona jambo hilo linafanikiwa kama ilivyokusudiwa na kufanya kazi usiku na mchana ili wananchi kupata huduma bora.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, aliwapongeza wawekezaji hao wazalendo kuamua kuwekeza nchini kutokana na kuvutiwa na mazingira ya Zanzibar.

Alisema serikali imeweka mazingira rafiki kwa wawekezaji kuwekeza Zanzibar katika sekta mbalimbali ambapo wizara yao imeanza kupokea wawekezaji mbalimbali kupitia sekta ya madini na nishati.

Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Iman Al -Jabry, alisema wameona kampuni yao ina uwezo wa kuisadia Zanzibar katika sekta za madini, maji na umeme na wana vifaa bora vitakavyotumika kwa ajili ya utafiti huku akibainisha kuwa kwa upande wa umeme, matarajio yao ni kuzalisha megawati 100 za umeme wa jua.

# Mwinyi, UN wateta hifadhi Mji Mkongwe

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekutana na ujumbe wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kujadili masuala kuhusu utunzwaji wa hifadhi ya kimataifa ya Mji Mkongwe.

Dk. Mwinyi alikutana na ujumbe huo Ikulu, Zanzibar, ukiambatana na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohammed Said pamoja na maofisa wa wizara hiyo.

Alisema licha ya maendeleo makubwa yaliyofikiwa na Zanzibar bado urithi wa hifadhi ya kimataifa ya Mji Mkongwe unaendelea kulindwa na kuenziwa kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa.

Rais Dk. Mwinyi alieleza ujumbe huo kwamba Selikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbalimbali za kuutunza urithi ikiwamo kuondosha msongamano wa maegesho ya vyombo vya moto kwenye maeneo yote ya Mji Mkonge ili kuenzi haiba ya mji huo kuendelea kuwa kivutio mashuhuri cha watalii na wageni wanaoutembelea mji huo.

Aidha, alisema katika kutekeleza hatua hiyo, serikali imeamua kujenga maegesho ya vyombo vya moto eneo la Darajani ikiwa njia mbadala ya kuondosha msongamano wa magari kwenye maegesho ya Mji Mkongwe.

Pia Dk. Mwinyi aliueleza ujumbe huo kwamba hatua nyingine iliyochukuliwa na serikali ni kushirikiana na sekta binafsi kuutunza urithi huo hasa kuyaendeleza majengo yaliyochakaa kwa kuyakarabati kwa mujibu wa kanuni na taratibu za kuyaenzi na kuyarudisha kwenye uhalisia wake. Alisema serikali inasimamia kwa karibu na kuhakikisha thamani na mali zote za asili zilizokuwemo kwenye majengo hayo zinarudishwa sehemu husika baada ya ukarabati.

Akizungumzia majengo ya Beit el Ajaaib na People's Palace, Rais Dk. Mwinyi alieleza ujumbe wa UNESCO kwamba serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano na serikali ya Oman zinaendelea kusimamia ujenzi wa majengo hayo.

Hata hivyo, Dk. Mwinyi alisema Beit el Ajaaib ni alama muhimu inayoitambulisha Zanzibar duniani kote.

Ujumbe huo wa UNESCO uliitaka serikali ya Zanzibar kuendelea kuuenzi na kuutunza urithi huo ili kuunusuru na athari za mabadiliko ya teknolojia ikiwamo kukua kwa maendeleo ya nyanja mbalimbali ambayo yanaweza kuwa sababu ya kubadili mandhari halisi na mwonekano wa mji huo.



Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Shreiner (kulia), akiteta jambo na Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada, Harjit Sajjan walipokutana katika Kongamano la Kimataifa la Women Deliver, jijini Kigali Rwanda juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapewa mbinu kuwania uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAWAKE wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi wametakiwa kuelewa mbinu sahihi za kufanya ushawishi ili kukabiliana na vikwazo vinavyowakwamisha kushika nafasi hizo katika ngazi mbalimbali.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar -SUZA, Dk. Salum Suleiman Ali, alisema hayo jana wakati wa mafunzo maalum kwa wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa.

Mafunzo hayo yana lengo la kuwajengea uwezo kutambua haki zao na kushiriki katika mchakato wa kugombea nafasi za uongozi kwenye vyombo vya uamuzi.

Akizungumza katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway Tanzania, alisema suala la kushiriki kugombea nafasi za uongozi ni mchakato endelevu unaohitaji maandalizi ya muda mrefu ili kujenga imani kwa jamii juu ya uwezo wa kiongozi katika kutetea na kusimamia changamoto zao.

Dk. Salum alisema ili wanawake kufanikiwa kushika nafasi za kisiasa na uongozi katika ngazi mbalimbali uwezo wa kujenga hoja na kuibua changamoto zinazowakabili wananchi ni mbinu muhimu katika kuongeza ushawishi wao kwa jamii.

Katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, Dk. Salum aliwataka wanawake kuanza kutumia fursa ya vyombo vya habari kuweka ajenda ya kuisemea jamii matatizo yao ili kusaidia kupata suluhisho.

Alisema vyombo vya habari ni daraja muhimu la kujenga uhusiano kati ya wananchi ambao ndio wapiga kura kwa ajili ya kufanya ushawishi utakaowavutia wapigakura.

"Lazima tuvitumie vyombo vya habari kwa ajili ya kufanya ushawishi wa mabadiliko kwa kutengeneza ujumbe na maudhui yanayolenga kuwasemea wananchi matatizo yanayowakabili. Hii itatusaidia kujijenga kisiasa na kuaminika kwa umma kuliko kusubiri uchaguzi umefika ndipo tuanze kujitokeza kutaka kuwasemea wananchi," alisema.

Pia alisema, TAMWA Zanzibar kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake katika masuala ya uongozi (SWIL) imechapisha mwongozo maalum ambao unatoa mwelekeo kwa wanawake kutambua mbinu za kutumia kushinda nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali.

"Tumeandaa kitini maalum kwa ajili ya kutoa muongozo kwa wanawake wagombea watarajiwa kujijengea uwezo wa kushiriki katika mchakato wa kugombea nafasi za kisiasa na uongozi pamoja na michakato yote ya kidemokrasia.

Mratibu wa TAMWA Zanzibar, Ofisi za Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema mafunzo hayo yamewashirikisha wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa na viongozi wa serikali za wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kati kwa ajili ya kuwaunganisha na kubadilishana uzoefu kuelekea kugombea nafasi mbali mbali za uongozi.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yanatolewa kwa wanawake kwa ajili ya kuwajengea ujasiri na uthubutu wa kuwa tayari kushiriki kugombea na kudai haki za wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Naye Saghira Moh'd Khalfan, mmoja wa washiriki hao, alishukuru TAMWA kwa kuandaa muongozo huo maalum kwa ajili ya kuwaonesha njia wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi na utawasaidia kwenye uchaguzi mkuu 2025 kukabiliana na changamoto zilizokuwa zikiwakatisha kufikia malengo yao kwenye uongozi.




**ROSE MHANDO**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 22, 2023



# WAMEIBA FURAHA?

BAADA ya wasanii nyota wa Bongo Fleva, Jux na Diamond platnumz, kutoa ngoma yao 'Enjoy' ambayo inaendelea kufanya vizuri, mjadala umeibuka kutokana na tuhuma ya kuiba kipande cha wimbo huo kutoka kwa wasanii wa Nigeria.

Malalamiko hayo yamezidi kushika kasi, huku Wanigeria wakisema baadhi ya nyimbo zinazopigwa na wasanii wa Kitanzania hasa Diamond, wameziiba kutoka kwa wanamuziki wa nchi hiyo.

Utata ulianza baada ya wimbo wa Enjoy ulioimbwa na Jux pamoja na Diamond, kufanana kabisa na ule wa Spyro kutoka Nigeria unaoitwa Who Is Your Guy?

Baadhi ya wadau wa muziki nchini wameonekana kutofautiana kuhusu tuhuma hizo, kuna wale wanaeleza kwamba tabia ya kuiba muziki ni kosa la msanii husika, na kuna wanaowatupia lawama maproduza kwa kufanya kazi hiyo.

Wanaokubaliana na hoja hiyo, wamedai kwamba msanii anapotaka kuandaa muziki wake ni lazima awe ameandaa wazo ambalo ndani yake inatokana na midundo ya muziki.

"Bongo Fleva imetawaliwa na wizi, ukisikiliza kwa makini utagundua wasanii wengi wanaiba muziki wa nje na kutungia mashairi. Hili jambo limezidi kuota mizizi na sasa tunapata aibu kama nchi kwa kuonekana tunaiba na hatuna uwezo wa kubuni, Alisema Shafii Salanda.

Hata hivyo, Shukuru Protus, amesema prodyuza ndio anatakiwa kulaumiwa kutokana yeye ndiye anatengeneza midundo na pengine anajua kabisa amechukua sehemu fulani.

## BASI SAWA

### Mafundi Amapiano hawa hapa



MUZIKI wa Amapiano kutoka Afrika Kusini unaendelea kutesa duniani, na sasa umekuwa kama alama ya burudani kwa vijana wengi.

Katika kutaka kuwadatisha mashabiki wa muziki huo hapa nchini, wasanii kutoka Afrika Kusini wanaojiita Shakes & Les wanatarajiwa leo kutumbuiza jijini Dar es salaam.

Miongoni mwa ngoma inayotamba ni Sikisi ambayo mashabiki wataweza kusikia live wakati wanamuziki hao watakapopanda jukwaani.

### Nyie mashabiki sasa mnapitiliza

MKALI wa Afrobeat kutoka Uganda, Spice Diana, amewapa ruhusa mashabiki zake kuwa na uhuru wa kumgusa sehemu yeyote wakati akitumbuiza.

Mrembo huyo alifichua haya baada ya mashabiki kuonekana wakimgusa sehemu zisizofaa wakati akiburudisha kwenye tamasha moja lilofanyika nchini humo.

Diana alionekana katikati ya mashabiki na kulazimika kusitisha uchezaji wake na kuwaonya mashabiki dhidi ya kumgusa mwili wake lakini haikusaidia waliendelea kumshika shika sehemu mbalimbali ya mwili wake.






## ROSE MHANDO NI MWENDO KASI

MKONGWE katika muziki wa Injili, Rose Mhando amekuwa msanii wa kwanza kwa muziki huo kufikisha wawafuasi milioni moja.

Rose ambaye kwa sasa anatamba na ngoma yake ya Secret Agenda aliyoitoa miezi saba iliyopita, amepata wafuasi hao kupitia mtandao wa You Tube.

Katika kitu cha kufurahisha wimbo huo umekuwa kinara kwa kutazamwa na watu milioni 13, tofauti na wasanii wengine wa muziki wa Injili nchini.



## Diambond usimfanyia hivyo

WANAMUZIKI nyota nchini, Diamond Platnumz na Zuchu wamesababisha mjadala mkali baada ya kuonyesha bahaba mazito wakiwa uwanja wa ndege wa jijini Dar es Salaam.

Wasanii hao walijikuta wakipeana busu zito kiasi ambacho kimewafanya watu kurudi tena kuwajadili kama kweli waliachana au ilikuwa kama njia ya kujiongezea umaarufu.

Wawili hao walirekodiwa na mtu mwingine alikuwa nyuma ya kioo, walionekana wakitembea kama mke na mume huku wakijadili jambo fulani na kisha walikumbatiana na kupigana busu zito.

## HII IMEENDA BWANA

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni mwezi Julai, waswahili wanasema ni mwezi wa saba ambao umevuka nusu ya mwaka 2023. Kwa sasa inatafutwa miezi mitano tu kuumaliza mwaka.

Kabla hata haujaisha, tayari miamba imeshakwenda studio na kutoa ngoma ambazo watoto wa mjini na vijana wa kisasa wanasema 'hii imeenda', wakiwa na maana imefanya vizuri.

Kwa bahati nzuri mwezi huu miamba imekutana. Wasanii wakubwa wametoa ngoma zao kila moja ikifanya vizuri.

**Diamond Platnumz ft Chley-Shu**

Anayechukuliwa kuwa msanii namba moja nchini, Diamond Platinumz, Julai 12 alifyatua ngoma moja kali aliyoiita 'Shu.'

Ngoma hiyo ameitoa akimshirikisha Chley Nkosi, mwanadada kutoka Afrika Kusini. Ni amapiano tu kwenda mbele.

**Ali Kiba-Sumu**

Mshindani wa Diamond kwenye masuala ya muziki, Ali Kiba siku mbili baada ya mwezake kuibuka na ngoma hiyo, yeye akaja na kitu kinaitwa 'Sumu.'

Ni kama walikuwa wanachunguliana, au wanafunzi waliokuwa shuleni mmoja akapelekea mtihani kwa mwalimu, naye akapeleka. Hayo ni mambo ya mwezi huu Julai.

**Kenny Sol ft Harmonize-One More Time**

Mtu anayewapa changamoto kubwa Diamond na Ali Kiba kwenye muziki wa bongo fleva, Harmonize yeye akashirikishwa kwenye ngoma ya msanii Mnyarwanda Kenny Sol iitwayo 'One More Time', ambayo imefyatuliwa Julai 12.

**Jux ft Diamond Platnumz**

Hili dude ni hatari tupu kwani kwa muda mfupi tu tangu litoke linaonekana limekubalika na mashabiki wa rika zote.

Ni Jux, akimshirikisha mkali Diamond Platnumz, ngoma inaitwa 'Enjoy.' Halafu ngoma yenyewe inachezeka kinoma.


"Bora niinjoi, maisha mafupi ni simpo ya nini niteseke roho, jiunge nani upoze koo." Ni baadhi ya meneno yaliyo kwenye pini hilo lililotoka Julai 14.

**Dogo Elisha ft Thomax-Tukilewaga**

Huyu ni mkali wa singeli, yeye ametoa ngoma yake kwa mfumo ya 'audio' iitwayo 'Tukilewaga.' Anazungumzia mazingira ya baadhi ya watu waliopata pesa mwisho wa mwezi na kwenda kupata kinywaji maeneo mbalimbali.

Yanazungumziwa pia mazingira pia ya baa au maeneo ambayo vinywaji vinapatikana.

"Leo tunalewa mwisho wa mwezi, madanga wote na machawa nimepokea mshahara, leo nipo mpaka majogoo maana pochi limetema, leo sikubali nikikosa danga naondoka na Zuwena, nawakubali mademu wa Buza maana meno yao ndiyo opena, fungua vizibo hatuondoki mapema, mama Amina mama Amina, kachanganya pombe kalewa mpaka kazima," anaimba Dogo Elisha kwenye moja kati ya 'vesi' zilizomo kwenye ngoma hiyo.



## FILAMU

# Kauli:Ulimi uliponza kichwa

**Na Adam Fungamwango**

ULIMI ni kiungo kidogo sana, lakini unaweza kusababisha jambo kubwa ambalo linaleta madhara kwa jamii.

Kwenye filamu ya 'Kauli' inaonyesha kuwa mtu anaweza kuongea jambo likasikika kwa jamii, baadaye kikatokea kitu ambacho aliyeropoka hawezi i kujitetea tena mbele za watu waliomsikia kwa mdomo wake.

Bakari Ndalahwa, aliyecheza kama Kenny anakorofishana na rafiki yake Ibra. Anachukua kisu na kwenda kumtishia kuwa atamuua. Anapaza sauti kuwa atamuua Ibra. Mwenzake anakimbia. Anarejea nyumbani kwake. Kesho yake Ibra anakutwa ameuawa kwa kisu. Ni kile kisu alichoshika Kenny alipokuwa anamtishia Ibra. Hata haukutumika upelelezi kugundua kuwa Kenny ndiye muuaji. Kila mmoja alisikia majibizano yale na ahadi ya kumuua Ibra.

Kenny akaanza kutafutwa kila kona. Hata hivyo anasema yeye hajaua. Lakini nani anaweza kuamini kama hajaua? Akaona bora aondoke, atoroke kabisa maeneo ambayo anajulikana.

Maafande wawili, Thomas na Eugin ndiyo wanapewa jukumu la kumsaka muuaji. Kenny anapigiwa simu na dada wa marehemu Ibra na kumlaumu juu ya mauaji hayo.

Akamjibu kuwa ni kweli kisu kilichotumika ni chake, lakini yeye hajaua na ameamua kufan ya upelelezi ili kujua kitu gani kilitokea baada ya ugomvi wao.

Maafande wawili wanafanikiwa kumkamata Kenny, lakini kwa namna ya ajabu anawatoroka na kwenda mafichoni. Huko anakutana na mtu ambaye anamjua muuaji halisi wa Ibra.

Lakini anataka apewe pesa, Kenny anamtafuta rafiki mwingine wa marehemu Ibra kumuomba msaada wa pesa ili amjue muuaji. Anapatiwa pesa hizo na kupeleka. Anashtuka anapoambiwa muuaji halisi. Anampigia simu afande Thomas awahi eneo husika. Anamfuata muuaji na kumpasha kuwa ametambua kuwa ndiye aliyemuua Ibra.

Muuaji anashangaa, lakini anakubali. Anamwambia amemuua kwa sababu amemdhurumu mzigo wa madawa ya kulevya aliyompa kwenda kuuza.

Na anamwambia kabisa kuwa alimuua kwa mkono wake na alitumia kisu chake kwa sababu alimuona siku alipokwaruzana na Ibra na kwenda kukiweka ndani na yeye akaenda kuoga, kitu kilichompa fursa kuingia ndani na kukichukua kabla ya kwenda kuua.

Muuaji aliongea hivyo akijua kabisa kuwa Kenny hatotoka hai sehemu ile walipokutania. Wakati anataka kumuua, afande Thomas akaingia na kumuweka chini ya ulinzi afande mwenzake Eugin. Kumbe ndiye muuaji. Upande afande, lakini upande muuza madawa ya kulevya.

Na yeye pamoja na mwenzake Thomas ndiyo waliopewa jukumu la kumsaka muuaji. Ni afande aliyekuwa akijisaka mwenyewe.



# Neo hatakagi kero

STAA wa shindano la Big Brother Naija, Neo Akpofure, amesema mahusiano yake yamevunjika kutokana na wanawake kuwa waongo.

Alipoulizwa kuhusu kuvunjika kwa uhusiano wake na wapenzi wake Oyinda na Sayo, amesema Mungu pekee ndiye anampenda mtu bila masharti, lakini kwake hawezi.

"Kwa kawaida, ningesamehe chochote, ningekusamehe kwa kunipiga usoni, imetokea hapo awali. Nikikuambia ningekusamehe kwa kunipiga, ina maana imeshatokea. nisamehe yote hayo, lakini jambo moja ambalo singekubali ni kuonekana mjinga na kukosa heshima. Kudanganya ni kukosa heshima kabisa." Amesema.



## Talaka nje nje Hollywood

WAIGIZAJI nyota wa Hollywood, Sophia Vergara na mumewe, Joe Manganiello, hatimaye wametengana baada ya kudumu kwenye ndoa kwa miaka saba.

Tangazo la kuachana limetolewa juzi, wakieleza msimamo wao na kutaka faragha katuika kipindi hiki ambacho hawako pamoja kama mke na mume.

"Tumefanya uamuzi mgumu wa kuachana. Kama watu wawili wanaopendana na kujaliana sana, tunaomba kwa upole heshima ya mtu mwingine. faragha yetu kwa wakati huu tunapopitia awamu mpya ya maisha yetu." Imesema taarifa hiyo.

## Kylie, Jordyn msiwachanganye

MARAFIKI wakubwa zamani Kylie Jenner na Jordyn Woods, wameibua mjadala baada ya kuonekana wakiwa pamoja baada ya miaka mitano wakiwa wamenuniana.

Ni mara ya kwanza kwa wawili hao kuonekana wakizurura pamoja tangu 2019, urafiki wao ulipokoma baada ya Woods kutuhumiwa kuwa na uhusiano na Tristan Thompson, ambaye ni mume wa Khloe Kardashian, dada wa Kylie.

Kulingana na mtandao wa TMZ, marafiki hao hawakuachana kutokana na skendo hiyo, bali waliamua kukaa pembeni kuacha wimbi hilo lipite.





## Kelvin Hart ziarani Rwanda

Mchekeshaji maarufu na muigizaji wa sinema nchini Marekani,Kevin Hart, amezulu Kumbukumbu ya Mauaji ya Kimbari ya Kigali na kutoa heshima kwa wahanga wa Mauaji ya Kimbari ya 1994 yaliyofanyika nchini humo.

Kumbukumbu ya Mauaji ya Kimbari ya Kigali, ni mahala ambapo miili ya watu 250,000 ya watu waliouawa.

Kulingana na gazeti la The New Times nchini humo, awali Haute Baso, alitembelea jumba la mitindo ya mavazi yanabuniwa na kutengenezwa Rwanda al maarufu Made in Rwanda, ambako alinunua mavazi.

## Ayra kumbe aibu imemvaa

MWANAMUZIKI staa wa Nigeria, Oyinkansola Sarah Aderibigbe, maarufu kama Ayra Starr, amesema siku ya kwanza kuonana na bosi wake alikuwa na aibu kumtazama usoni.

Mrembo huyo mwenye umri wa miaka 21, amesema bosi wake, Don Jazzy ndiye mtu mzuri zaidi kuwahi kutokea katika maisha yake.

Alikiri kwamba mwanzoni alikuwa na aibu alipokutana na mtayarishaji huyo wa muziki aliyepata mafanikio, lakini kadiri muda ulivyosonga, aligundua kuwa alikuwa mtu mtulivu.



# Nape asisitiza taarifa zilizochakatwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema Rais Samia Suluhu Hassan anatamani kuona watanzania wakipewa taarifa nzuri na zilizochakatwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, hasa katika kipindi hiki ambacho diplomasia ya uchumi inavyofanya kazi kubwa. Hayo aliyasema jana jijini Arusha katika hafla ya uzinduzi wa Shahada ya Media Unuwai na Mawasiliano kwa Umma katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA). "Nilipokuwa ninakuja hapa niliwasiliana na Rais Samia na kumpa taarifa ya uzinduzi huu, amefurahi sana na kuwapongeza. Anatamani kuona Watanzania wakipata taarifa sahihi, nzuri na zilizochakatwa vizuri kwenye vyombo vya habari na mitandao yetu ya kijamii,"alisema.

Nape alisema Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kutangaza Tanzania huko duniani na kuvutia wawekezaji katika maeneo mbalimbali yaliyopo, hivyo kupitia mafunzo hayo wanaamini watapata wataalam wa habari watakaoieleza dunia fursa zilizopo. Nape alisema IAA ni chuo cha kwanza Tanzania kutoa kozi hiyo tofauti na vingine ambavyo vinatoa Shahada ya Media pekee au ya mawasiliano ya umma, hivyo anaamini wataalamu watakaozalishwa watakuwa bora na wakipekee watakaokidhi mahitaji ya soko.

"Huko mtaani tuna wataalamu wanaozalishwa na vyuo vingine kidogo soko linapata tabu. Lakini ninaamini hapa mmefanya utafiti na kuanzisha kozi hii kulingana na mahitaji ya soko na hawa wataisaidia nchi yetu kupata wataalamu watakaokidhi mahitaji ya soko, sababu watafahamu dunia na nchi inataka nini. "Uzalishaji na ulaji wa maudhui na vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii, inategemea sana maendeleo ya sayansi na teknolojia ya habari, hivyo huu ndio uamuzi sahihi wa busara kwa kuunganisha mambo haya mawili na kutoa shahada moja,"alisema.

Nape alisema uanzishwaji wa mafunzo hayo ni moja ya suluhu ya kumaliza changamoto za baadhi ya vijana walioingia katika tasnia ya habari hasa ya mitandao ya kijamii na kukiuka maadili ya habari kwa kupata elimu. Alisema wanapoangazia tasnia ya habari na mawasiliano, wanahitaji wataalamu walioandaliwa vizuri ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwenye sekta ya habari na ufumbuzi wa teknolojia.

"Teknolojia inapokua kuna madhara mengi yakiwamo ya kupoteza tamaduni zetu, lakini kupitia wataalam hawa tunaamini wataingia katika tasnia hii wakifahamu miiko na umuhimu wa kudumisha haya yote na kutoa habari zenye tija kwa nchi yetu,"alisema.

Nape alitoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari hasa waliopo Arusha kupeleka wafanyakazi wao katika chuo hicho, kwa ajili ya kupata mazoezi kwa vitendo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Greyson Msigwa, alishukuru kuanzishwa kwa kozi hiyo chuoni hapo akiomba ziwapo na zile zinazotolewa kwa muda mfupi ili kuwezesha waliopo kazini na waliosoma muda mrefu kujifunza mabadiliko yanayotokea katika sekta hiyo. Mkuu wa Chuo, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema katika mwaka wa masomo 2023/2024, wanatarajia kuanzisha kozi mpya tano zikiwamo nne za Shahada na moja ya Shahada ya Uzamili.

"Kuanzishwa kwa kozi hizo kunafanya IAA kuwa na jumla ya kozi 71, ambapo kati ya hizo, 16 ngazi ya cheti, 17 Stashahada, 24 Shahada na kwa upande wa Shahada za Uzamili ni kozi 14," alisema.

Prof. Sedoyeka alisema kwa shahada hiyo mpya ya Media Unuwai na Mawasiliano kwa Umma itakuwa ni daraja kati ya uandaaji, uchakataji na utoaji wa maudhui ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii wa zamani na wa kisasa, kuunganisha msingi wa taalama na mawasiliano na mwelekeo wa kisasa wa teknolojia ya habari.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa pili kulia), akizindua rasmi programu ya Shahada ya Media Anuwai na Mawasiliano kwa Umma katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), juzi. Wengine ni Mkuu wa chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka (kulia) na Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho, Dk. Mwamini Tulli (wa pili kushoto). **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wafugaji wafurahia hati za kimila

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

MAKABILA ya Wasonjo (Batemi) na jamii ya wafugaji wa Kimasai, yanayoishi Tarafa za Loliondo na Sale, Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, yameeleza namna yanavyouona mwanga mpya katika mpango wa upimaji wa ardhi yao, kwa kuwa sasa wanaamini hati za kimila zitarejeshea tabasamu lao.

Kutokana na mpango huo, viongozi wa mila wa jamii hizo za kifugaji, wameomba serikali kuwatambua na kuwapa ushirikiano ili kumaliza migogoro mbalimbali inayowakabili.

Jana, viongozi wao walieleza shauku yao kuhusu suala la umiliki wa ardhi, wakati wa mafunzo maalum ya haki ya kisheria ya umiliki wa ardhi kwa kutumia hati ya kimila.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Taasisi ya Tanzania Pastoralist Community Forum (TPCF) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Kiongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai eneo la Loliondo (Laigwanani), Salinge Manyinyi, alisema baada ya kupewa elimu kuhusu mchakato wa uwekaji mipaka kwenye baadhi ya maeneo katika eneo lao, wameelewa utaratibu wa kumiliki ardhi kwa hati ya kimila, tofauti na awali.

Alisema kuwa licha ya uelewa huo, baadhi ya watu au taasisi binafsi, zimekuwa zikipotosha kuwa Loliondo hali sio nzuri, kwamba hakuna uhusiano mzuri baina ya viongozi hao wa kimila na serikali, jambo ambalo alilikanusha.

Kiongozi wa mila wa jamii ya Wasonjo katika Kata ya Samunge, Mwanamije Fungayo, alisema suala la kumiliki ardhi kwao ni muhimu, hivyo wanasubiri hati za kimila ambazo zitawasaidia katika maisha yao.

"Tupo tayari kushirikiana na viongozi wa serikali ngazi zote, tusikubali upotoshwaji unaofanywa na baadhi ya watu au taasisi ambazo zinaangalia maslahi, tumeelewa manufaa ya kupimwa ardhi yetu na faida zake, kwani tutapata hata hati za kimila," alisema Fungayo.

Ofisa Tarafa ya Loliondo, William Ndossi, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, alisema serikali itashughulikia ombi hilo na wapo tayari kutoa ushirikiano, kwa sababu wanajua umuhimu wa viongozi hao wa kimila.

Alisema serikali inaendelea na juhudi ya kupunguza migogoro ya ardhi kwa wananchi, lakini pia kuangalia hata kwa wanawake wa jamii hiyo kuweza kumiliki ardhi na kunufaika nayo. Mkurugeni wa Taasisi ya TPCF, Joseph Ole Persambei, alisema taasisi hiyo itafanya utaratibu wa vitambulisho kwa viongozi hao wa kimila.

Alisema kusajiliwa kwa viongozi hao kutawezesha waweze kutambuliwa na serikali, lengo ni kuweza kuwatambua wale ambao wanajiita viongozi wa kimila wakati siyo kweli.

# Waziri ataka taarifa wachangiaji wa kampeni ya GGM Kili Challenge

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ummy Nderianga, ameagiza Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), kupeleka ofisi kwake taarifa ya wanufaika wa uchangiaji wa Kampeni ya GGM Kili Challenge ili kujua ushiriki wa sekta binafsi katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Agizo hilo alilitoa jana wakati alipokwenda katika lango la Mweka la Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), kuwapokea mashujaa 61 waliojitolea kupanda Mlima Kilimanjaro, kuhamasisha kampeni hiyo ya kuchangia fedha.

Kati ya mashujaa hao, 36 walipanda mlima huo kwa kutembea na 25 waliendesha baiskeli kilomita zaidi ya 400 kuuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Alisema anataka kuona taarifa hiyo ikionyesha mashujaa hao wamefanya nini katika kampeni mbalimbali kila mwaka, ili kuonyesha Watanzania namna ambavyo nchi inapinga unyanyapaa na lengo la kufikia sifuri tatu ifikapo mwaka 2030.

"Tunawapongeza mashuja wote, mafanikio yenu yanadhihirisha kuwa mwitikio wa mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI unakwenda vizuri. Iwapo kutakuwa na dhamira ya dhati kwa kila mmoja wetu na ushirikiano wa pamoja wa kufikia malengo ya kitaifa ya kufikia Sifuri tatu, tutakuwa tumefanikiwa zaidi," alisema.

Naibu Waziri huyo, alisema serikali imeweka lengo ambalo kila wizara na taasisi ya umma inatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya masuala ya VVU na UKIMWI.

Alisema katika mwaka 2022/23, TACAIDS ilitengewa Sh. bilioni 14.98 kwa ajili ya masuala ya hayo na mwaka huu wa fedha imetengwa Sh. bilioni 25.86.

"Kupitia mwongozo wa kudhibiti VVU/ UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza mahali pa kazi katika sekta ya utumishi wa umma, wizara, idara na wakala wa serikali, zimeweka masuala hayo kwenye sera zao kisekta.

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOKWENDA

# Dar es Salaam ilipokuwa ikichemka kama bahari kila 'wikiendi' enzi hizo

Na Adam Fungamwango

MWANAMUZIKI nguli nchini, Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki' ambaye kwa sasa ni mgonjwa, akiwa amejipumzisha nyumbani kwake maeneo ya Mtoni jijini Dar es Salaam.

Kwanza kabisa tumpe pole na kumuombea kwa Mungu apone na maradhi yanayomkabili.

Moja ya vibao vyake vikali alivyovitoa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ni ule uanoitwa 'Mtoto wa Mjini.'

Wimbo huu unaeleza kila kitu. Unaeleza jinsi wakati huo Dar es Salaam ilivyokuwa ikichemka kama bahari. Ni kwamba pamoja na wakazi wengi wa Dar es Salaam kuwa na kazi maalum za kufanya kutokana na kuwa na mashirika mengi binafsi na ya umma, lakini pia walipenda mno starehe ya muziki wa dansi.

Kiki anasema bendi zimetapakaa kila kona ya Dar. Kumbi za starehe ziko za kutosha maeneo yote. Pia watu wajaa kwenye kumbi zote hizo, kana kwamba wanaingia bure.

Msanii wa hip hop, Profesa Jay, yeye mwanzoni mwa miaka ya 2000, alikuja na ngoma yake aliyoita 'Bongo Dar es Salaam' Moja kati ya mistari yake ni ile inayosema 'Sinza ya leo kila nyumba baa, na zote zinajaa, na hapo ndipo utakaposhangaa.'

Hivi ndivyo kumbi za burudani zilivyokuwa zikijaa kila wiki. Leo tutaziziangalia kumbi za jijini Dar es Salaam tu. Ipo siku tutazingumzia za mikoani pia.

Hapa unaweza kushangaa kitu kimoja tu. Zamani Dar haikuwa na watu wengi kama ilivyo sasa. Inakadiriwa kuwa miaka ya 1970, hadi katikati ya miaka ya 1990 kuliwa na wakazi laki tano mpaka milioni moja. Pamoja na uchache huo, kumbi zaidi ya 100 jijini Dar es Salaam zilikuwa zinajaa. Watu walikuwa wanajua kutumia. Watu walijua kujirusha. Walijua kula bata. Wanafanya kazi wiki nzima, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili ilikuwa ni siku ambazo wengi walikwenda kuburudika dansini.

Kwa sasa Dar inakadiriwa kuwa na watu kiasi cha milioni tano, na baa zimekuwa nyingi mno kuliko hata mwanzo. Lakini kwa bahati mbaya sana bendi si nyingi tena kama zaidi, kwani kulikuwa na bendi zaidi ya 50 za watu binafsi, Mashirika ya Umma, Makapuni, Jumuiya za Chama cha Mapinduzi, na majeshi yote ya ulinzi na usamala.

Kutokana na bendi nyingi kupiga kwenye kumbi mbalimbali wakati huo na kutangazwa na gazeti moja tu wakati huo la Uhuru na Jumapili, gazeti la Mzalendo, ingawa baadaye likaja pia gazeti la Mfanyakazi.

Bendi na mageti haya kwa kiasi kikubwa yalisababisha kumbi nyingi jijini Dar es Salaam kuwa maarufu sana. Na hii ni kutokana na watu kutaka kujua bendi gani itapiga wapi na lini. Ilikuwa haiwezekani kutambua hilo bila kupata magazeti hayo.

Haikuzifanya kumbi au baa hizo kuwa maarufu wakati huo, lakini majina hayajafutika kwenye vichwa na mashabiki wengi wa muziki wakati huo ambao kwa sasa baadhi wako Dar na wengine wapo mikoani wakiendelea na harakati zingine za maisha.

Baadhi ya kumbi zilizotikisa wakati huo kwa bendi mbalimbali kwenda kupiga muziki wa dansi ni Ruvuma Mpaka Maputo Bar, iliyokuwa maeneo ya Vingunguti kuelekea Kipawa, wenyewe waliipachika jina la 'Njia Panda kwenda Air Port.'

Kumbi zingine zilizovuma na kutetemesha Dar na hatoweza kufutika kirahisi kwenye akili ya mashabiki wa muziki wa miaka hiyo ni ,Madison Square (Tabata), Maghorofani (Tandika), Makonde Bar (Msasani), Mbwisi Bar (Manzese), Mkirikiti Bar (Msasani), Muleba Bar (Mabibo), Mundo Bar (Temeke), Mzalendo Pub (Ilala) Amana Social Club (Ilala), Miembeni Bar (Ilala), Mundo Bar (Temeke), New Mazulia (Vingunguti), Ndendeule Bar (Mtoni), Omax Bar (Keko), Sabasaba Bar (Mbagala), Safari Resort (Kimara), Sensera Bar (Tandika), Silent Inn (Mwenge), Super Stereo Bar (Temeke), Super Fanaka Bar (Buguruni), Super Mini (Temeke), Tumaini Social (Kiwalani), Uhemeli Bar (Luhanga), Wami Bar (Mwananyamala), White House (Ubungo) First Inn (Mburahati), Kigogo Lodge, na Waluwelu Bar (Kiwalani).

Zingine ni CCM Kata 14 (Temeke), CCM Kata ya 14 Temeke, Highway Bar (Kurasini), Bondeni Bar (Kariakoo), DDC Keko, DDC Kariakoo, DDC Magomani Kondoa, Dimax Bar (Tandika), Friends Corner (Manzese), Hotel 92 (Shekilango), Hunters Bar (Ubungo), Ikweta Bar (Mtoni), Kigongo Bar (Buruguni), Makonde Bar (Mikocheni), Muleba Bar (Mabibo), Uhemeli Bar (Luhanga) na Wami Bar (Mwananyamala).

Historia ya ukumbi huu ni kwamba bendi nyingi zilikuwa zinapiga, lakini bendi pendwa zilikuwa mbili tu, kwanza kabisa Juwata Jazz Band ambayo ilikuwa ikipiga hapo mashabiki hufurika ndani hadi nje, lakini pia Super Matimila chini ya hayati Dk. Remmy Ongalla.

DDC Mlimani Park waka Sikinde waliwahi kupiga mara chache, lakini kilichowapata, waliamua tangu siku hiyo kusikitisha kupiga ukumbi wa Wami Bar. Ipo siku nitasimulia kisa hiki.

Kumbi zingine ni, Mpakani Bar baadaye ikaitwa, Silent Inn (Mwenge), Stereo Bar (Kinondoni), White House (Ubungo) uliokuwa ukitumiwa na Maquiz du Zaire, Shirikisho Bar (Vingunguti), Kwa Mama Bar (Vingunguti), Chabruma Inn, Chimoka Bar (Magomeni) kwa sasa inaitwa 'Traventine', Lang'ata Bar (Kinondoni), Jemelasi Bar 'Mtoni kwa Aziz Ally'. Pandia Bar (Buguruni) na Top Life Bar (Kinondoni Mkwajuni), Kimboka By Night na Sewa Bar (Buguruni).

Hizi ni kwa uchache tu kati ya kumbi nyingi za Dar es Salaam zilizokuwa zikipokea bendi mbalimbali.

Unaweza kukuta kila kumbi ina bendi kwa siku moja. Bendi Dar es Salaam kama nilivyosema zilikuwa nyingi mno, zingine zilikuwa zikitoka hata mikoani kwenda Dar kwani tayari zilikuwa zina mashabiki wengi kwa sababu ya nyimbo zao ambazo walizirekodi na kutamba sana redioni.

Bendi ziligawana mashabiki. Kuna zilizojaza sana. na zingine zilizopata mashabiki wa wastani. Lakini bendi karibu zote zinapata mashabiki. Hii ndiyo Dar iliyoliyokuwa ikichemka kama bahari kama alivyoimba King Kiki.



Wanamuziki wa bendi ya Nuta Jazz 'Msondo Ngoma', ambayo baadaye ilijulikana kama Juwata Jazz, Ottu Jazz na Msondo Ngoma Music band wakiwa jukwaani mwishoni mwa miaka ya 1970.




Wanamuziki, Michael Bilal wa DDC Mlimani Park Orchestra akiwa na gitaa la solo (kulia) na Abdallah Gama, akipiga gitaa la rhythm wakiwa jukwaani na bendi hiyo miaka ya 1980.




Basi lililokuwa likitumiwa na wanamuziki wa bendi ya DDC Mlimani Park Sikinde Ngoma ya Ukae enzi hizo kupeleka kwenye maonyesho na kuwarudisha majumbani.

# Mwanajeshi wa Marekani aliyekimbilia Korea kaskazini atambulika ni mtoro

**WASHINGTON,** MAREKANI

WIZARA ya Ulinzi ya Marekani, imeeleza kwamba inamchukulia mwanajeshi Travis King, aliyevuka mpaka na kuingia Korea kaskazini, kuwa ni mtoro.

Maelezo ya wizara hiyo ilieleza kwamba inatambua King kuwa hayuko kazini na wala likizo wakati akiendelea kushikiliwa Korea Kaskazini.

Maofisa wa wizara hiyo, pia walikiri kwamba, hawakuwa na habari kuhusu hali yake au mahali alipokuwa akishikiliwa.

Awali, Ikulu ya White House ilisema Marekani ilijaribu kuwasiliana na Korea Kaskazini kupitia njia nyingi lakini haikupata jibu.

King alikimbia na kuvuka eneo la mpaka lenye ulinzi mkali siku ya Jumanne.

Haijulikani ikiwa ameasi au anatarajia kurudi baada ya kufanya tukio hilo la hatari.

Tovuti ya habari yenye makao yake mjini Washington ya Messenger, ilisema kuwa imeona ripoti ya ndani ya serikali ya Marekani ambayo ilieleza matendo ya King mara alipovuka mpaka.

Ilinukuu ripoti hiyo ikisema King alikimbia hadi kwenye jengo upande wa Korea Kaskazini.

Inasemekana aligonga mlango kwa nguvu, na wakati hakukuwa na jibu, alikimbia kuzunguka nyuma na kuingia kwenye gari.

Kisha mara moja akasafirishwa, kulingana na tovuti.

Wataalamu wanasema mwanajeshi wa ngazi ya chini kama huyo atakuwa na thamani ndogo ya kijasusi na propaganda kidogo, ambayo inaweza kusababisha Korea Kaskazini kumwachilia, lakini kitakachomtokea bado hakijafahamika.

Christine Wormuth, mkuu wa Jeshi la Marekani, alielezea wasiwasi wake mkubwa kwa Travis King na jinsi anavyoweza kutibiwa.

Aliambia Jukwaa la Usalama la Aspen kuwa kuna hofu kuhusu hali yake.

Mgogoro huo unawadia wakati nchi hizo mbili zinavutana kuhusu amani ya rasi ya korea. Uhusiano na Marekani umeporomoka katika miaka ya hivi karibuni, baada ya Korea kaskazini imefanya majaribio mengi ya makombora yenye nguvu zaidi yanayoweza kubeba vichwa vya nyuklia.

Marekani imetoa ushauri wa onyo kwa raia wake wanaosafiri hadi nchini humo ikiitaja kama moja ya taifa hatari duniani.

**BBC**

# Upinzani Kenya, wanadiplomasia wa nje wafanya mazungumzo

**NAIROBI,** KENYA

WAKATI Kenya imezizima kwa maandamano ya siku tatu mfululizo, mmoja wa viongozi wakuu wa Muungano wa Azimio La Umoja One Kenya, Kalonzo Musyoka, amefanya mkutano wa faragha na wanadiplomasia.

Mkutano huo ulifanyika nyumbani kwake , jijini Nairobi jana. Aidha, kikao hicho kinakuja kukiwa na hali ya wasiwasi miongoni mwa mataifa ya nje na mashirika ya kigeni kuhusu kuenea kwa ghasia na kupoteza maisha ya watu wakati wa maandamano ya kupinga serikali.

Haijajulikana ni nini hasa kilichozungumzwa kati ya Kalonzo na wanadiploamasia wa kigeni Taarifa zilisema kuwa wanadiplomasia hao walikuwa ni kutoka Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya, Marekani na Denmark.

Mapema wiki hii wanadiplomasia kutoka Marekani, Uingereza, Canada, Ujerumani na nchi nyingine tisa waliutaka Muungano wa Azimio la Umoja na serikali kutatua tofauti zao kwa amani.

Wakati huo huo, kiongozi wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga amesema anaugua mafua makali ambayo yalimpata mwanzoni mwa maandamano ya kupinga serikali.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha NTV kwa njia ya simu, Odinga hata hivyo alisema anaendelea vyema na kuongeza kuwa kutoonekana kwake na kutoshiriki kwa viongozi wengine wakuu wa upinzani katika maandamano hayo kunamainisha ni maandamano ya Wakenya.

"Maandamano sio ya baba, ya Martha au ya Kalonzo au ya mtu mwingine. Maandamano ni ya Wakenya wote", alisema Odinga Maandamano hayo yameitishwa na upinzani kupinga gharama ya juu ya Maisha na muswada wa fedha wa 2023 uliozuiwa na mahakama baada ya bunge kuunga mkono.

Hata hivyo, Rais William Ruto amesema kwamba serikali yake itaendelea kulinda usalama na demokrasi ya taifa la kenya kwa hali na mali.

Mashirika ya haki za binadamu yametaja idadi ya waliofariki katika maandamano nchini Kenya kufikia watu 30 tangu maandamano ya kuipinga serikali yaanze wiki mbili zilizopita.

**BBC**



Moja ya mtambo wa kurushia makombora ya Cluster uliopelekwa nchini Ukraine hivi karibuni**. PICHA: BBC**

# Marekani yathibitisha mabomu 'Cluster' yaanza kutumika Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imethibitisha kuwa Ukraine imeanza kutumia mabomu hatari aina ya cluster dhidi ya vikosi vya Russia nchini humo.

Msemaji wa Usalama wa Kitaifa John Kirby, alisema maoni ya awali yanaonyesha kuwa mabomu hayo yanayotawanyika yanatumiwa ipasavyo kwenye nafasi za ulinzi za Russia wakati wa operesheni.

Mabomu aina ya cluster hutawanya mabomu mengi na yamepigwa marufuku na zaidi ya mataifa 100 kutokana na kuwa na hatari kwa raia.

Marekani ilikubali kuyasambaza ili kuongeza silaha kwa Ukraine. Ukraine nayo iliahidi mabomu hayo yatatumika tu kuwaondoa wanajeshi Russia.

"Wanayatumia ipasavyo," alisema Kirby. Aliongeza "Wanayatumia ipasavyo na ukweli ni kwamba yana athari kwa safu ya ulinzi ya Russia hasa katika ujanja wao wanaotumia. Nadhani naweza kuachia hapo."

Marekani iliamua kutuma mabomu ya kutawanyika baada ya Ukraine kuonya kwamba inaishiwa na silaha wakati wa mashambulizi yake ya majira ya joto, ambayo yamekuwa ya polepole na ya gharama zaidi kuliko wengi walivyotarajia. Rais Joe Biden aliita uamuzi huo kuwa mgumu, huku washirika wake Uingereza, Canada, New Zealand na Hispania wakipinga matumizi yake.

Idadi kubwa ya silaha iliyotumwa ni mizinga yenye kiwango cha chini cha asilimia 2.35 cha kutolipuka.

Silaha hizo ni nzuri zinapotumiwa dhidi ya wanajeshi kwenye mahandaki na maeneo yenye ngome, kwani zinatawanyika eneo kubwa na kuwa hatari sana kusogea kutoka eneo moja hadi jingine.

Russia imetumia mabomu kama hayo ya kutawanyika nchini Ukraine tangu ilipoanzisha uvamizi wake kamili mwaka jana.

Akijibu uamuzi wa Marekani wa kutuma mabomu hayo, Rais wa Russia Vladimir Putin, alisema nchi yake ina silaha zinazofanana na hizo na zitatumiwa ikiwa zitatumika dhidi yao. Oleksandr Syrskyi, Jenerali wa Ukraine anayesimamia operesheni mashariki mwa nchi hiyo, aliiambia BBC wiki iliyopita kwamba vikosi vyake vinahitaji silaha zitakazosababisha uharibifu mkubwa kwa wanajeshi wa aridhini wa adui.

**BBC**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakiboresha huduma ya majisafi katika Kata ya Kwembe, Ubungo mkoani Dar es Salaam jana, kupitia mpango maalum wa kutatua changamoto ya msukumo mdogo wa maji na ukosefu wa huduma kwa baadhi ya maeneo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**




Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa (UoI), Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Andrew Mbwambo (kulia), akionyesha baadhi ya kazi za wanafunzi wanaosomea elimu ya ujasiliamali katika chuo hicho kwa wananchi waliotembelea maonyesho ya 18 ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akisalimiana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Cameroon, Felix Mbayu alipomtembelea ofisini kwake, jijini Yaounde nchini Cameroon jana. **PICHA: BUNGE**



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma (wan ne kulia), akikabidhi hati miliki ya kiwanja kwa mmoja kati ya wananchi 266 waliokabidhiwa hati hizo katika kijiji cha Kilapula, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dk. Jumaa Mhina (wa tano kulia) na (kulia) ni Mkurugenzi wa kampuni ya Makazi Solutions (T) Ltd, iliyopewa zabuni ya upimaji ardhi wilayani humo, Selemani Pazzy. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, SACP Henry Mwaibambe akionyesha baadhi ya simu kwa waandishi wa habari jana, zilizotumiwa na wezi wa mitandaoni mkoani humo, baada ya kuwakamata watuhumiwa 11 wakiwa na vifaa mbalimbali walivyokuwa wakivitumia kutekelezea uhalifu wao. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Anna Shinini akizungumza na wanawake kuhusu masuala ya ujasiriamali ili kukuza uchumi wao, alipotembelea Kata ya Emboreet, juzi. **PICHA: GIFT THAD**EY

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-18

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Kabla ya kufika maeneo ya Kawe Ukwamani sehemu ambayo kulikuwa na miti miti hivi na majani, Eddy akamuomba dereva akaweke gari pembeni ili akajisaidie."

Hakuwa na hiana, akafanya hivyo tena huku akiendelea kupiga stori ikionekana kama wameshazoena na stori za michezo zimenoga.

Alifikiria kuwa mlango ungefunguliwa ili abiria wake atoke kujisaidia. Haikuwa hivyo. Badala yake akasikia bega likiguswa kwa nguvu kidogo.

Alichodhani ni kwamba abiria wake ameshindwa kufungua mlango, hivyo aligeuza sura ili ahakikishe kama ndivyo hivyo kabla hajapekeleka mkono wake nyuma kumfungulia.

Alichokiona hakuamini. Ni kama alikuwa anaota ndoto ya jinamizi. Alichokishuhdia ni mdomo wa bastola iiyokuwa imeelekezwa kichwani.

"Rudisha uso wako mbele, haraka sana." Haikuwa sauti ile waliyokuwa wanaongea habari za Simba na Yanga.

Ni kama aliyeongea ni mtu mwingine sana. Hali hiyo ilimtisha dereva. Alirudisha sura yake mbele.

"Nyoosha mikono juu." Aliamriwa na kutii.

"Mimi ni mtu mzuri sana, wala sina haja ya kukudhuru, na wala si nia yangu. Ninachotaka unijibu maswali yangu machache tu, ukinijibu kwa ufasaha bila uongo au hadaa nitakuachia urudi nyumbani uendelee na maisha na familia yako. Lakini kama ukiniongopea na kunisumbua, nitatawanya ubongo wako."

Dereva alikuwa kimya asiamini kile kilichomtokea na anachosikia.

Eddy alitoa simu yake na akafungua video fupi ile aliyotumiwa na Maria ambayo aliinyonya kutoka kwenye kamera za CCTV za Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

Akaiweka mbele ya dereva taxi huku mkono mmoja bado ukiwa umeshika bastola.

Hakuongea kitu chochote, alitaka dereva huyo ajione mwenyewe anavyompokea mgeni yule na kuondoka naye hadi eneo ambalo kamera haikuweza tena kurekodi.

"Huyo ni nani?" Eddy akauliza kwa utulivu.

"Mimi." Akajibu bila kupepesa macho.

"Na huyo mwingine?"

"Alikuwa ni abiria wangu."

"Unaikumbuka siku hii?"

"Ndiyo naikumbuka."

"Sasa ili urejee salama nyumbani kwako, urudi kwa mkeo na watoto wako, naomba ukanionyeshe sehemu ambayo abiria wako huyu aliposhukia au ulipompeleka."

"Sawa mzee ngoja nikupeleke."

Akazima na kurudisha simu yake janja mfukoni.


"Kumbuka usijaribu kuniongopea, bahati nzuri mimi ukiniongopea nafahamu."

Hakukuwa na kwenda kujisaidia wala nini. Ilikuwa ni mbinu tu aliyotumia Eddy ili gari lisimame, kwani hakutaka kumtolea bastola wakati anaendesha gari.

Kuna mazingira ambayo kama mpelelezi unalazimika kufanya hivyo, lakini huwa ni hatari kwani anaweza kuyumbisha gari na hata kutokea ajali kwa woga ambao dereva anaweza kuingiwa nao.

Mazingira ya wakati ule kwake yalikuwa tulivu na hakukuwa na ulazima sana wa kufanya hivyo kwa sababu dereva alikuwa raia wa kawaida tu, na si wale ambao ni maharamia, au majambazi.

Alitii amri, akapiga stati na kugeuza gari. Safari ilianza, lakini wakati huu haikuwa tena kama ile ya mwanzo. Ya mtu na abiria wake kuongea kama mtu na rafiki yake wakipiga stori za hapa na pale hasa zile za soka, Simba na Yanga.




**"Mimi ni mtu mzuri sana, wala sina haja ya kukudhuru, na wala si nia yangu. Ninachotaka unijibu maswali yangu machache tu, ukinijibu kwa ufasaha bila uongo au hadaa nitakuachia urudi nyumbani uendelee na maisha na familia yako. Lakini kama ukiniongopea na kunisumbua, nitatawanya ubongo wako."**

Safari hii ilikuwa ni mtu na mateka wake. Hakuwa na stori wala kuguna ndani ya gari. Kila mmoja alikuwa akifikiria kivyake.

Dereva aliirudisha gari mpaka kutoka barabara ya Kawe, kuingia ya Bagamoyo, akatafuta lami hadi maeneo ya Mwenge, kwenye makutano ya barabara ya Bagamoyo na Sam Nujoma.

Aliiacha barabara ya Bagamoyo na kuanza kuifukuzia ya Sam Nujoma. Eddy wala hakutaka kumuuliza wanakwenda wapi. Alichojua tu ni kwamba anapelekwa pale ambapo alimshusha abiria yule aliyemkodisha baada ya kushuka kutoka kwenye ndege iliyotua kutoka Mwanza zaidi ya miezi sita iliyopita.

Gari ilitafuna lami na kuacha maeneo ya Ubungo, Tabata na Buguruni hadi Tazara. Ilionekana kabisa wanarejea tena Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Ni kweli walifika hadi Kipawa na kuukuta uwanja wa ndege, lakini sasa walipitiliza. Ndipo Eddy alipojua kuwa siku ya tukio gari ilienda maeneo ya Ukonga kuelekea juu Gongolamboto na wala haikuelekea mjini.

Walipofika maeneo ya Ukonga Banana waliachana na barabara kubwa ya lami, wakakata upande wa kulia ambako kulikuwa na barabara ambayo mwanzo ilikuwa na lami chakavu, lakini mbele haikuwepo kabisa.

Walikata kona nyingi zilizochosha kiasi cha Eddy kwa mara ya kwanza akamuuliza swali dereva.

"Huku ndipo wapi?"

"Kwa Mapunda."

Baadaye gari lilisimama. Tayari mishale ya saa ilionyesha saa tano usiku.

"Nyumba ile pale." Dereva alionyesha kwa kidole nyumba moja iliyokuwa mbele yao kando ya barabara waliyokuwa wanapita.

"Okay, sasa pita ili niione vizuri kwa mbele. Alifanya hivyo na Eddy akawa anaipiga picha na kuirekodi kupitia simu mbili tofauti. Moja ilikuwa na kazi ya kupiga picha, lakini nyingine kurekodi video fupi.

Aliporidhika akamuamuru dereva kuondoka haraka. Akafanya hivyo.

"Unaelewa nini kuhusu mtu huyu uliyomleta hapa?"

"Nachoelewa kuwa ni mteja wangu tu."

"Ni mara ngapi anakukodisha?"

"Mmh, ni zaidi ya mara tano au sita hivi." Dereva alikuwa akijibu huku akiendesha gari.

"Mara zote ilikuwa ni kutoka uwanja wa ndege kumleta hapa tu?"

"Ndiyo, ila mara moja ilikuwa ni kumtoa kituoni Ukonga Banana kumpeleka Magomeni.

"Siyo hapa nyumbani huwa unamleta?"

"Hapana."

"Alikuwa na nani?"

"Alikuwa na watu wawili."

"Walikwambia wanakwenda wapi na kufanya nini?"

"Hawakuniambia, ila walikuwa na mzigo."

"Mzigo wa nini?"

"Sikuwauliza, ila walionekana kama wamenunua mzigo hivi, wakauweka kwenye buti, nikawapeleka hadi Magomeni, mimi nikarudi zangu."

"Walikupigia simu kutoka uwanja wa ndege?"

"Ndiyo, na kwasababu mimi huku napafahamu, jamaa aliniambia atakuwa madukani ananunua mzigo, hivyo nisiende nyumbani kwake tutakutana kituoni."

"Ilikuwa saa ngapi?"

"Saa tano ya usiku yaani kama saa hizi."

Ingawa dereva alikuwa anajibu kwa kifupi kile tu anachokifahamu, lakini alikuwa hafahamu kuwa majibu yote aliyokuwa akijibu yalikuwa muhimu mno kwa Eddy, yalimuongezea vitu vingi ambayo vilionekana kumpa mwanga wa tukio zima la mauaji ya Tessy.

"Sasa sikiliza nikwambie. Usimwambie mtu yoyote kuhusu jambo hili. Kuanzia nilipokukodisha hadi hapa tulipofika. Na nasema hivi kwa usalama wako. Yoyote utakayemwambia basi utakuwa ndiyo mwisho wako. Na siyo kama mimi nitakuua, huyo au hao utakaowaambia watakumaliza. Kuwa mwangalifu, mimi ni mtu mzuri tu. Yoyote atakayekusumbua, piga simu

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KMKM YAANZA KUJIWINDA KUELEKEA MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, KMKM SC wameanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na michuano hiyo ambayo imepangwa kufanyika kuanzia mapema mwezi ujao.

KMKM ndio mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar itautumia Uwanja wa Azam Complex katika mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKMK, alisema tayari timu hiyo imeingia kambini na msimu huu imejipanga kufika mbali katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka.

"Kikosi chetu kimeshaanza mazoezi rasmi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya CAF pamoja na Ligi Kuu Zanzibar, tutataka kuona tutasonga mbele kwa kupata matokeo mazuri katika mechi zote mbili tutakazocheza," alisema Msimu.

Kocha huyo alisema lengo la kuanza mazoezi mapema ni kufanya wachezaji wazoeane na kurekebisha mapungufu yatakayoonekana tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao.

Aliongeza KMKM inayapa umuhimu mkubwa mashindano hayo ya kimataifa na ndio sababu benchi la ufundi limependekeza kufanya usajili wachezaji wapya watakaokiongezea nguvu kikosi chao.

"Tumependekeza kusajili wachezaji wapya watano ambao watakuja kuiongezea nguvu timu yetu hasa katika mashindano ya CAF ambayo yanatukabili, hasa nafasi ya ulinzi, tunataka beki wa kati lakini pia tunahitaji mshambuliaji atakayetusaidia katika safu hiyo, " Msimu aliongeza.

Katika kujiweka imara, alisema kikosi chao kinatarajia leo kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya KMC FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tutaimarisha kikosi chetu kwa kufanya mazoezi na kucheza mechi mbalimbali za kirafiki, Jumamosi (leo) kuanzia saa 2:00 asubuhi tutajipima na KMC ya Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Mao," aliongeza kocha huyo.

Aliongeza anaamini mchezo huo utampa taswira juu ya maandalizi yake yalipofikia na namna ambavyo anahitaji kuboresha kikosi wakati bado dirisha la usajili wa wachezaji halijafungwa.

# Kikapu Pwani kuanza Julai 30

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya kikapu ya Mkoa wa Pwani imepangwa kufanyika kuanzia Julai 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Tumbi uliopo Kibaha, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Kikapu Mkoa wa Pwani (CRBA), Abdallah Mpogole, alisema lengo la ligi hiyo ni kupata timu zitakazoshiriki mashindano ya taifa.

Mpogole alisema maandalizi ya ligi hiyo yako katika hatua za mwisho na wanatarajia kuona ushindani kutokana na maandalizi ya muda mrefu yaliyofanywa na timu zilizothibitisha kushiriki.

"Ligi hii ni muhimu sana kwa sababu itatusaidia kupata timu zitakazoshiriki mashindano ya ngazi ya taifa, vile vile tunaendelea kuutangaza mchezo huu hapa mkoani," alisema Mpogole.

Katibu huyo alisema ligi hiyo inafanyika kwa mara ya kwanza na wanawaomba wadau wa mchezo huo kutoa ushirikiano ili Pwani ifikie malengo ya kupata wawakilishi imara.

Alizitaja timu tatu ambazo zitachuana kuwa ni pamoja na Tumbi Survivors, Kibaha Centipedes na Termites Kings.

"Bado tunaendelea kufanya mazungumo na baadhi ya kampuni kwa ajili ya kufanikisha jambo letu, kikubwa kupitia ligi hii vijana watajitangaza na kupata nafasi ya kuonekana," aliongeza Mpogole.




Mshambuliaji wa Azam FC, Abdul Suleiman 'Sopu' (mbele), akipambana kuwania mpira dhidi ya Sospeter Bajana wa timu hiyo katika mazoezi yaliyofanyika Tunisia jana. Azam imeweka kambi nchini humo kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa 2023/2024. **PICHA: MTANDAO**

## Chabruma aula JKT Queens

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa JKT Queens umemtangaza mshambuliaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Esther Chabruma, kuwa kocha mpya wa mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, imefahamika.

Chabruma amechukua mikoba iliyoachwa na Ally Ally ambaye msimu uliopita alifanikiwa kuiongoza timu hiyo kutwaa ubingwa bila ya kupoteza mchezo hata mmoja.

Ofisa Habari wa JKT Queens, Masau Bwire, alisema lengo la kufanya mabadiliko katika benchi la ufundi ni kuhakikisha wanajenga kikosi imara pamoja na kufanya usajili bora kuelekea msimu mpya.

Masau alisema wanataka kuona timu yao inapeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itakayofanyika mwezi ujao lakini pia kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake wanaoshiriki.

"Usajili umefanyika vizuri, wachezaji wetu wote wapya na waliosalia tutawatambulisha siku yetu maalum, na siku hiyo tutawaaga wachezaji wa timu yetu ya JKT Queens wanaokwenda Uganda katika mashindano ya CECAFA, sisi ndio wawakilishi wa Tanzania kwa upande wa klabu mwaka huu," alisema Bwire.

Aliongeza kikosi cha timu hiyo kiko kambini Kigamboni kwa ajili ya kujiandaa na mashindano hayo na matarajio yao makubwa ni kutetea kombe hilo ambalo msimu uliopita lilichukuliwa na Simba Queens.

"Tunaendelea vyema na maandalizi, kila kitu kinakwenda vyema, tunataka kuendeleza kile kilichofanywa na Simba Queens msimu uliopita, tutalinda heshima ya Tanzania katika michuano hiyo ya CECAFA ya wanawake," alisema Bwire.

Mashindano hayo ya CECAFA yanafanyika kwa mara ya tatu wakati msimu wa kwanza yalifanyika Kenya na wenyeji, Vihiga Queens walitwaa taji hilo huku Simba Queens ikimaliza katika nafasi ya nne.

Hata hivyo mwaka jana katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Simba Queens iliishia hatua ya nusu fainali na wenyeji ASFAR ya Morocco ikitwaa ubingwa mbele ya Mamelodi Sundowns Ladies.

## ZISIKUPITE

### KANE AIGOMEA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane (29), hatasaini mkataba mpya na Tottenham Hotspur. Kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na miamba ya Ligi Kuu Ujerumani,Bayern Munich.**(Times)**

### DANJUMA KUTUA EVERTON

WINGA wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Arnaut Danjuma, mwenye umri wa miaka 26 anatazamiwa kujiunga na Everton kwa mkopo kutoka Villarreal. **(Sky Sports)**

### DIABY SAFARI IMEIVA

KLABU ya Aston Villa imefikia makubaliano na Bayer Leverkusen kwa ajili ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Moussa Diaby, mwenye umri wa miaka 24. **(Birmingham Live)**

### LUIZ, GALLAGHER SOKONI

KLABU ya Tottenham Hotspur imewatambua kiungo wa Aston Villana Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa Chelsea, Conor Gallagher (23), kama wachezaji ambao huenda wakachukua nafasi ya Pierre-Emile Hojbjerg, raia wa Denmark ambaye yuko katika mazungumzo ya kujiunga na Atletico Madrid. **(Mail)**

### BORGES ANUKIA WEST HAM

WEST Ham inakaribia kushinda mbio za kumnunua, Carlos Borges wa Manchester City, ambaye pia anasakwa na Borussia Dortmund na Eintracht Frankfurt, baada ya kutoa pauni milioni 14 kwa winga huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 19. **(Guardian)**

### BARCOLA KUMRITHI MAHREZ

MANCHESTER City inamfikiria mshambuliaji wa Lyon Mfaransa, Bradley Barcola, mwenye umri wa miaka 20 kama mbadala wa Riyad Mahrez ambaye anatarajia kuondoka klabuni hapo. **(90 Min)**

### UNITED, PSG VITANI

KLABU ya Manchester United iko tayari kuwasilisha ombi lao la ufunguzi kwa Atalanta ili kumnunua mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund, mwenye umri wa miaka 20, ambaye pia anasakwa na PSG. (**Fabrizio Romano**)

### MANE KUTUA AL NASSR

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Senegal, Sadio Mane, mwenye umri wa miaka 31, amefikia makubaliano ya maslahi binafsi ya kujiunga na klabu ya Al-Nassr ya Saudi Aarabia. **(90 Min)**

### SILLA KUINOA AL AHLI

KOCHA wa Fulham ambaye ni raia wa Ureno, Marco Silva, mwenye umri wa miaka 46, amepewa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 40 kwa ajili ya kuinoa klabu ya Saudi Arabia, Al-Ahli. **(Sky Sports)**

### PARTEY ANUKIA SAUDIA

KLABU ya Al-Ahli ya Saudi Arabia inalenga kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal ambaye ni raia wa Ghana, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 30. **(Mail)**

### JULIO KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inakaribia kufikia makubaliano ya pauni milioni 15 na Fiorentina kwa ajili ya kumnunua beki wao raia wa Brazil, Igor Julio, mwenye umri wa miaka 25. **(Telegraph)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES NAHODHA MPYA RASMI UNITED

Ni kutokana na kuiongoza vyema timu katika msimu uliopita na...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, ametajwa kuwa ndiye nahodha mpya wa Manchester United, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imetangaza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atachukua nafasi ya beki, Harry Maguire, ambaye alivuliwa unahodha wa timu na Kocha, Erik ten Hag, baada ya nyota huyo wa kimataifa wa England kushindwa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Fernandes ana mabao 64 na asisti 54 katika michezo 185 kwa klabu hiyo katika michuano yote, na msimu uliopita alitumia muda mwingi wa kiongoza timu wakati Maguire akiwa benchi au kuumia.

ESPN iliripoti Mei 31, mwaka huu United iko tayari kusikiliza ofa kwa Maguire msimu huu wa joto na kutarajia nia kutoka kwa West Ham, ambao walifanya uchunguzi kuhusu kupatikana wake wakati wa dirisha la usajili la Januari iliyopita.

"Kiungo huyo wa Ureno tayari ameshavaa kitambaa cha unahodha wa United mara nyingi na Ten Hag amethibitisha sasa ataiongoza timu hiyo kwa misingi ya kudumu," ilisema taarifa ya United.

"Kama nahodha, mshindi huyo mara mbili wa tuzo ya Sir Matt Busby kama Mchezaji Bora wa mwaka wa klabu, ataendelea kuiongoza United ikipigania mafanikio katika msimu wa 2023-24."

Fernandes alikosolewa kwa uchezaji wake duni wakati United wakichezea kichapo cha mabao 7-0 kutoka kwa wapinzani wao Liverpool hapo Machi, mwaka huu.

Kampeni ya United ya kujiandaa na msimu mpya inaendelea, na kikosi hicho cha Old Trafford kiliifunga Lyon ya Ligi Kuu Ufaransa bao 1-0, mechi iliyochezwa Jumatano iliyopita.

Baadaye United ilisafiri hadi Marekani, ambapo itamenyana na Arsenal, Wrexham, Real Madrid na Borussia Dortmund katika mechi za kirafiki kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

HABARI MICHEZO

# NEYMAR: NILILIA SIKU TANO, TULIPOAGA KOMBE LA DUNIA




**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR amesema "nililia kwa siku tano mfululizo" baada ya Brazil kutolewa katika mashindano ya Kombe la Dunia 2022 na kuongeza alifikiria kustaafu kucheza kimataifa baada ya kushindwa kwenye hatua ya robo fainali dhidi ya Croatia.

Fowadi huyo wa Paris Saint-Germain mwenye umri wamiaka 31, hajaichezea nchi yake tangu kupoteza kwa penalti Desemba 9, mwaka jana.

Neymar aliiweka Brazil mbele kwa kile kilichoonekana kama bao la ushindi katika muda wa nyongeza kabla ya Croatia kusawazisha zikiwa zimesalia dakika tatu na kushinda mikwaju hiyo na kutinga nusu fainali.

"Siwezi kukwambia kilichopita kichwani mwangu," alisema Neymar akiiambia YouTuber Casimiro.

"Kulikuwa kushindwa kwa uchungu zaidi katika maisha yangu, kwa hakika. Nililia kwa siku tano mfululizo. Iliniumiza sana, ndoto yangu ilikuwa imebadilika. Tukiwa 0-0 nilifunga bao, walisawazisha na tukapoteza kwa penalti. Ni maumivu ambayo wachezaji na wafanyakazi pekee wanaweza kuelewa.

"Ulikuwa wakati mbaya zaidi maishani mwangu. Ilionekana kama mazishi, mtu analia upande, mtu mwingine akilia upande mwingine. Ilikuwa hali ya kutisha, hisia ile sitaki kuiona tena."

Neymar ameichezea Brazil katika fainali tatu za Kombe la Dunia akianza mwaka 2014, 2018 na 2022.

Mwaka 2014 waliadhibiwa 7-1 na washindi Ujerumani katika nusu fainali kwenye ardhi ya nyumbani kwao baada ya fowadi huyo kuumia mgongo katika raundi ya awali.

Miaka minne baadaye nchini Urusi, Brazil ilichapwa 2-1 na Ubelgiji katika robo fainali kabla ya kuondolewa katika hatua hiyo na Croatia nchini Qatar mwaka 2022.

Katika mahojiano na CazeTV, Neymar alisema alikuwa akifikiria kustaafu kimataifa baada ya kukatishwa tamaa, lakini sasa yuko tayari kucheza tena 2026.

"Baada ya Kombe la Dunia (2022), kwa kweli sikutaka kurejea katika timu ya taifa ya Brazil," alisema.

"Lakini nimebadilisha mawazo yangu. Kwa sababu nina njaa sana. Nilibadilisha mawazo yangu.

"Baada ya Kombe la Dunia, sikutaka kupitia uchungu wa kupoteza tena. Kuona familia yangu ikiteseka sana, hilo linanielemea sana. Lakini itabidi wavumilie tena. Itakuwa vizuri. Lazima iwe hivyo."

Kampeni ya Brazil ya kufuzu Kombe la Dunia 2026 itaanza Septemba mwaka huu.

Shirikisho la soka la Brazil, CBF, limemteua Fernando Diniz wa Fluminense kama kocha wao mpya wa muda kwa mkataba wa mwaka mmoja, huku wakimfuatilia Carlo Ancelotti wa Real Madrid kama uteuzi wa muda mrefu.

Neymar amerejea katika mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya na PSG, ambayo sasa inafundishwa na kocha wake wa zamani kule Barcelona, Luis Enrique.

Jana Ijumaa walicheza na Le Havre katika mechi ya kirafiki kabla ya kuondoka kwa ziara nchini Japan ambako watacheza na Al Nassr, Cerezo Osaka na Inter Milan.

# Mane kumfuata Ronaldo Al Nassr

**MUNICH, Ujerumani**

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Sadio Mane, amefikia makubaliano ya maslahi binafsi ya kujiunga na klabu ya Al Nassr inayoshiriki Ligi Kuu Saudi Arabia (Saudi Pro Leagues), vyanzo vimeithibitishia 90min.

Nyota huyo wa zamani wa Liverpool amekuwa ni mmoja wa wachezaji wa hadhi ya juu wanaohusishwa na kuhamia Mashariki ya Kati katika dirisha hili la usajili.

Mane anarejea katika msimu mbaya wa kwanza akiwa na Bayern Munich, akifunga mabao 12 katika michezo 38 katika michuano yote na alijizolea umaarufu alipoingia katika ugomvi na mwenzake, Leroy Sane, baada ya kupoteza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

90min iliripoti Mei mwaka huu, Bayern Munich wangemuuza Mane, ingawa mwanzoni alikataa kuhamia Saudi Arabia.

Steven Gerrard alitaka kuzungumza naye kwa nia ya kumtaka katika Ligi Kuu ya Saudia baada ya kuchukua mikoba ya kuinoa Al Ettifaq, lakini sasa amefikia makubaliano ya msingi na Al Nassr ya Cristiano Ronaldo.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni kubwa, huku Mane akisisitiza hakufikiria kuhamia Saudi Arabia.

Bayern wanaamini kuwa hawataweza kupata pauni milioni 35 walizolipa kumsajili Mane kutoka Liverpool, lakini watajaribu kiasi kinachokaribiana na hicho.



# Onana apewa jezi namba aliyoizoea

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imetangaza namba ambayo atavaa golikipa wao mpya, Andre Onana, waliyemsajili kutoka Inter Milan juzi.

Raia huyo wa Cameroon alikamilisha uhamisho wake kutoka San Siro hadi Old Trafford Alhamisi jioni, na mara moja akasafirishwa na watazamaji wapya kwenye ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani baada ya kusaini mkataba wa awali wa miaka mitano.

Onana atakuwa mlinda mlango mpya wa United baada ya mkataba wa nguli wa klabu hiyo, David de Gea, kumalizika.

Alitarajiwa kurithi jezi namba moja ya Mhispania huyo, chaguo la kawaida kwa makipa wengine - lakini amechagua namba tofauti.

Badala yake, Onana atavaa jezi namba 24 kwani ndio ambayo amekuwa akivaa mara nyingi katika maisha yake ya klabu kubwa, akiivaa Ajax na Inter Milan.

Alichukua namba moja kwa muda katika msimu wa 2017/18 wa Ajax kabla ya kurejea namba 24 mwaka mmoja baadaye.

Namba 24 ni ya thamani, na ni magwiji wa zamani wa klabu ya United wameivaa hapo zamani.

Onana ndiye mchezaji wa kwanza wa Mashetani Wekundu kuchukua 24 tangu beki ,Timothy Fosu-Mensah, ambaye aliondoka kwenda Bayer Leverkusen mwaka 2021.

HABARI MICHEZO

# AZAM YATAMBA ITAREJEA NYUMBANI IKIWA 'MOTO'

**Na Abdallah Mataka**

LICHA ya timu yake kupoteza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Esperance de Tunis ya Tunisia, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssoupha Dabo, amesema anafurahi timu yake kupata nafasi ya kujipima na timu 'ngumu'.

Azam FC iko imeweka kambi yake Tunisia kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Matajiri hao wa Chamazi, Dar es Salaam pia watachuana kuwania Ngao ya Jamii na Kombe la FA.

Dabo aliliambia Nipashe kuwa anaendelea kukijenga kikosi chake na sasa wanajipanga na mchezo mwingine wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya US Monastir utakaochezwa leo.

Alisema kupitia mechi hizo, atapata nafasi ya kuangalia uwezo wa kila mchezaji wake na kupata kikosi chake cha kwanza.

"Nimehitaji kucheza mechi ngumu ili nifahamu kikosi changu kinatakiwa kujengwa zaidi katika nafasi gani, mechi hizo zitasaidia wachezaji wangu kuimarika na kupata uzoefu wa kutosha," Dabo alisema.

Naye Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema timu yao inaendelea vizuri na maandalizi kuelekea msimu mpya wa 2023/2024 na anaamini watarejea nchini wakiwa na makali zaidi.

Ibwe alisema kocha wao ametaka kucheza mechi dhidi ya wapinzani wenye uwezo zaidi ili kuwapa wachezaji wake uzoefu kuelekea msimu mpya wa mashindano.

"Tukimalizana na US Monastir, mechi nyingine tumebaki nazo ni dhidi ya Etoile du Sahel, CS Sfaxien, zote za Tunisia, tunaamini tukirejea nyumbani, tutakuwa hatushikiki," alisema Ibwe.

Ikirejea nchini, Azam FC itakutana na Yanga katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.



Mshambuliaji wa Yanga, Stephano Aziz Ki (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na Tamasha la Siku ya Mwananchi litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. PICHA: MTANDAO

# Dodoma Jiji yajichimbia Iringa

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI vikosi vya timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu vikianza kambi, kikosi cha Dodoma Jiji kimeelekea Iringa kwa ajili ya kufanya maandalizi yake ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, amesema timu yao imeweka kambi Iringa ambapo pamoja na mambo mengine, wanafurahia kufanya mazoezi katika hali ya hewa ya baridi.

"Hali ya hewa ni nzuri, uwanja mzuri, yaani yale mahitaji yote ya 'pre season' tuliyokuwa tunayahitaji yanapatikana hapa na ndiyo maana tumechagua kuja Iringa, kulikuwa na sehemu kama tatu tulizipendekeza, lakini mwisho wa siku hapa ndipo tumepachagua kwa sababu imekidhi vigezo," alisema Liogope.

Kocha huyo alisema pia wachezaji wote wapya ambao waliwatangaza kujiunga na kikosi chake wameshawasili na kuanza mazoezi, isipokuwa nyota baadhi ambao wanasubiri kumalizana nao.

"Bado hatujamaliza kusajili, kuna baadhi ya wachezaji tunamalizana nao, mambo yakishakuwa tayari nao watajiunga na sisi," alisema kocha huyo.

Nyota wapya ambao tayari klabu hiyo imewatangaza kuwasajili ni beki wa pembeni, Simon Gustavo, Mtenje Albano wote kutoka Coastal Union na winga kutoka Ihefu SC, Idd Kipangwile.

## Yanga njooni 'tuinjoi'

INATOKA UK. 24

kikosi cha kwanza na badala yake atachanganya wachezaji ili kuona kile alichowapa mazoezini ndani ya siku 10 walizokuwa katika maandalizi.

Naye mchezaji mpya wa Yanga, Mahletse Makudubela 'Skudu', alisema amejipanga vizuri kuelekea mchezo huo wa kirafiki na anaimani itakuwa mechi nzuri na yenye kuvutia.

Skudu alisema ushindi katika mchezo wa leo sio kipaumbele chao na kikubwa ni kuonyesha benchi la ufundi baada ya kipindi kifupi walichofanya mazoezi ya pamoja.

"Mafanikio waliyoyapata yamekuwa kivutio na kujiunga na timu hii licha ya klabu nyingi kunihitaji, sasa nipo kuisaidia Yanga kwa msaada wa wachezaji wenzangu," alisema Skudu ambaye amepewa jezi namba sita ambayo ilikuwa ikivaliwa na Feisal Salum 'Fei Toto'.

Alisema viongozi walimwambia wamemchagulia jezi hiyo iliyokuwa inavaliwa na mchezaji mkubwa na yeye kwa sababu anapenda changamoto ameamua kuivaa.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema matayarisho yote yamekamilika huku kukiwa na burudani ya wasanii maarufu na wanaotamba na ngoma zao mpya kwa sasa akiwamo Jux, Marioo, Rayvanny, na wa muziki wa singeli wakiongozwa na Sholo Mwamba na Dula Makabila.

"Matayarisho yamekamilika, tuna mambo makubwa matatu, namba moja ni kuhakikisha wanachama, mashabiki na Watanzania wote wanaokuja uwanjani wanakuja 'kuinjoi' mchezo mzuri wa timu hizi mbili, Yanga na Kaizer Chiefs, kitu kilichonifurahisha, wamekuja wote kamili, kikosi chao chote cha wachezaji tegemeo wengine wamewasajili msimu huu, " alisema Kamwe.

Wachezaji wapya watakaotambulishwa leo ni pamoja na Pacome Zouzoua, Kouassi Yao wote raia wa Ivory Coast wakisajiliwa kutoka Asec Mimosas, Maxi Mpia Nzengeli Mkongomani kutoka Maniema FC, Gift Fred (SC Villa ya Uganda) na Skudu aliyekuwa Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

Kwa upande wachezaji wazawa waliosajiliwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni Nickson Kibabage kutoka Singida Fountain Gate (zamani Singida Big Stars) na Jonas Mkude, aliyeachwa na watani zao, Simba.

## Simba: Tumesajili timu ya makombe

INATOKA UK. 24

Sadio Kanoute, Fabrice Ngoma na Nassor Kapama.

Wekundu wa Msimbazi kwa sasa kiko Uturuki kikifanya maandalizi ya msimu mpya na itarejea nyumbani tayari kwa utambulisho wa kikosi chake katika Tamasha la Simba Day 2023 litakalofanyika Agosti 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumamosi Julai 22, 2023

Nipashe




## Fernandes nahodha mpya rasmi United

KURASA 21

## Simba: Tumesajili timu ya makombe

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitambulisha rasmi jezi yake mpya itakayotumika katika msimu wa 2023/2024, mabosi wa timu hiyo wamesema hawajakurupuka katika mchakato wa usajili na kila mchezaji waliyemnasa, basi uamuzi wake umetokana na malengo maalumu.

Juzi Simba ilitangaza kuwanasa wachezaji wapya watatu, wote raia wa Tanzania ambao ni straika, Shabani Chilunda, beki wa kati, Hussein Kazi na kiungo mkabaji, Abdallah Hamisi, ambaye amewahi kucheza soka la kulipwa Kenya.

Meneja Habari wa Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema hawajakurupuka kuwasajili wachezaji hao, bali wamefanyika mchakato mkubwa kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi ili nyota hao na wengine wawe msaada katika kikosi chao.

"Tuna michuano mingi sana safari hii, Ngao ya Jamii, Super League, Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la Mapinduzi, Kombe la FA, Ligi ya Mabingwa Afrika na mingine itakayojitokeza, lazima tuwe na kikosi kipana kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya mara kwa mara, badala ya kuchezesha wachezaji wale wale," alisema Ahmed.

Aliongeza usajili huo ni matekelezo ya Kocha Mkuu Roberto Oliveira 'Robertinho' ambaye aliagiza kuelekea msimu ujao anataka kila namba iwe na wachezaji wawili au watatu wenye uwezo unaofanana au kukaribiana.

Chilunda, straika wa zamani wa Azam FC amesajiliwa kwa mkataba wa miaka miwili akiwa mchezaji huru, akiwa amewahi kuzichezea klabu za CD Tenerife na CD Izarra zote za Hispania na Moghreb Tetouan ya Morocco.

Nyota huyo anatarajia kwenda kuwania namba dhidi ya John Bocco, Jean Baleke na Mzambia Moses Phiri.

Kazi, aliyetokea Geita Gold na kuwahi kuzichezea klabu za Mbeya Kwanza, Polisi Tanzania na soka la kulipwa, Shelisheli, anakwenda kupambania namba dhidi ya Henock Inonga, Kennedy Juma na Che Fondoh Malone, huku Hamisi, Mtanzania ambaye amecheza soka la kulipwa nje ya nchi kwa muda mrefu kwenye klabu za Muhoroni Youth FC, Sony Sugar, Bandari FC zote za Kenya atachuana dhidi ya Mzamiru Yassin,

INAENDELEA UK. 23

UZI MPYA



Wachezaji wa Simba, Henock Inonga (kushoto), Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' na Che Fondoh Malone, wakiwa wamevaa jezi mpya za timu hiyo zilizozinduliwa rasmi katika kilele cha Mlima Kilimanjaro mkoani, Kilimanjaro jana. **PICHA: SIMBA SC**

# YANGA NJOONI 'TUINJOI'

## ●●● Gamondi aahidi mechi nzuri akiivaa Kaizer Chiefs, Marioo, Jux...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HII Imeenda, ndio kauli mbiu iliyokuwa ikitumiwa na Yanga kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi ambayo itahitimishwa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs FC kutoka Afrika Kusini itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tamasha hilo pia ni sehemu maalum ya kuwatambulisha wachezaji wapya waliosajiliwa kwa ajili ya msimu mpya wa mwaka 2023/24 ambao utaanza kwa mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii kwa kukutana na Azam FC, mechi ikichezwa Agosti 9, mwaka huu.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema mechi ya leo itakuwa nzuri licha ya kutopata muda mzuri wa maandalizi akieleza siku 10 alizokuwa na kikosi hicho huku baadhi ya wachezaji kuchelewa kujiunga na kambi hazikumtosha.

Gamondi alisema watajitahidi kuonyesha kiwango bora dhidi ya vigogo hao wa Afrika Kusini na analazimika kufanya kazi kwa presha wajitahidi kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Kupata ushindi katika mchezo huo itasaidia kujenga morali ya wachezaji wangu, lakini matokeo ya michuano iliyopita ya Kombe la Shirikisho Afrika imekuwa ni changamoto kwetu kwa sababu watahitaji kuonyesha kiwango kizuri kama ilivyo hapo awali.

Mchezo huu pia utanisaidia katika maandalizi ya ligi, iwe nimeshinda au nimepoteza, muhimu kutazama wachezaji kama wameshika mbinu na kile nilichowapa katika uwanja wa mazoezi," alisema Gamondi.

Aliongeza hana uzoefu na ligi ya Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati lakini atahitaji zaidi kujifunza na kuwataka wachezaji kuonyesha vipaji vyao kwa muda mfupi waliokuwa pamoja.

Kocha huyo alisema leo hatatumia

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >